MWONGOZO WA MSTAHIKI MEYA.

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

SURA YA PILI

MUHTASARI WA MAONYESHO

SEHEMU 1

Onyesho 1

Onyesho la kwanza linalotokea Zahanatini wakati wa jioni. Kuna vilio vya watoto vinavyosikika kwa umbali. Daktari Siki anaonekana aliye na wasiwasi, asiyetulia huku akiwa amevalia mavazi yake rasmi. Wasiwasi wa Siki unatokana na hali ilivyo pale zahanatini ambako kuna wagonjwa wasioweza kuhudumiwa kutokana na ukosefu wa dawa. Waridi anamwelezea Siki kuwa wagonjwa ni wengi kuliko siku iliyotangulia, naye Siki anashangazwa na hali hiyo kwani hakuna dawa zahanatini. Waridi ansema kuwa ameulizia akaelezewa kuwa shehena ya dawa ipo bahari kuu nab ado haijawasili nchini. Zipo ila zipo katika bahari kuu.

Kwa hivyo Meya amesema kuwa wawashauri wagonjwa wasubiri kwani baada ya siku tatu dawa zitakuwa tayari zimeisha kuwasili bandarini na siku tatu hivi baada ya kuwasili watakuwa wamezipokea hospitalini. Siki haamini mambo haya. Hata hivyo,

anaamua wawashughulikie wagonjwa ambao dawa zao zinapatikana; wale ambao dawa za kuwafaa zipo tayari.

Tatizo ni kuwa hawana hela za kulipia huduma wanazotaka na wengine hawana hata karatasi ya kunakilia udodosi wao kwani hawana pesa. Waridi anasema kuwa nchi yenyewe ni masikini hali ambayo Siki hakubaliani nayo. Punde tu anaingia mama mmoja na motto mgonjwa mkononi. Mtoto huyo anaendesha tangu jana jioni baada ya chajio. Chakula hicho alikitoa anakofanya kazi, kwa *Mstahiki Meya*.

Chakula chenyewe ni wali kwa maharagwe kiporo yaani yaliyolala. Mama hakukitokosa chakula hicho tena nyumbani kwani hana moto, makaa siku hizi yamepanda bei tangu sheria ya misitu ishike kasi, na vilevile bei ya mafuta taa inapanda kila uchao. Inadhihirika wazi kuwa tatizo la motto huyu ni la utapia mlo, jambo ambalo linamshangaza Waridi.

Siki anawalaza wagojwa hospitalini ili kuwapa matumaini tu, kwani hakuna dawa. Waridi anaandaa mchanganyiko wa sukari na chumvi katika maji moto, hata ingawa anajua kuwa si matibabu. Siki anaamua kuwalaza wale wagojwa walio nje wakisubiri bila kulipa, hasa wale wanaolemewa kwani wote ni wafanyakazi wa *jiji*, jinsi hospitali yenyewe ilivyo *jiji*.

Waridi anaposisitiza kuwa wale wenye kulazwa walipie, Siki anapinga akisema kwamba kitanda si dawa, na kuwa zile dawa anazoahidi huenda zikawa ni kauli tu zinazoanguliwa katika matamshi. Onyesho 1 linaisha Siki akiwa amekata tama, naye Waridi akimshauri kuwa si vizuri kushuku wanayoambiwa bali wasubiri kwa kutumaini.

Onyesho II

Ni siku ya pili nyumbani kwa Meya. Meya yuko mezani ambako kina mayai kadhaa kwenye sahani, na kikombe chai. Meya anapoinua kikombe cha chai kuinywa, inamchoma. Meya anamuita Gedi ambaye anaingia mbio nusura aanguke.

Anasimama wima na kupiga saluti. Meya anamwamuru Gedi amwite Dida, ambaye vilevile anapoulizwa maswali kwa hamaki, anamjibu kwa upole. Meya anamzomea Dida kwamba ametumwa kumchoma kwa chai.

Lakini Dida anamuomba msamaha kwa unyenyekevu. Meya analalama kuhusu mayai madogo na jinsi Dida alivyomruhusu anayeyaleta kumpunja kwa kuleta viyai vidogo. Hatimaye anatoa amri kuwa anayeleta mayai asiwahi kuleta tena.

Gedi anarejea kwa Meya na habari kuwa Daktari Siki angependa kuonana naye. Meya anakubali kumwona Siki, huku akiwa na wasiwasi. Siki amekuja na habari za hali ya maisha ya watu wanaomlilia Meya na wanaotaka awasikilize kuhusu hali yao ya maisha ambayo ni ngumu. Siki anasema kuwa watu hawa wameshindwa kumudu gharama za matibabu na dawa zenyewe hakuna, gharama za maisha zimezidi kupanda na mahitaji nayo yanazidi kuongezeka ilhali mishahara haiongezekikipandi. Lakini Meya anapinga hali hii na kusema kuwa hakuna Baraza lenye uthabiti kama lao katika ujirani wao.

Siki analalamika shida za watu wa Cheneo wengine wanakufa kwa njaa kwa sababu hawawezi kumudu mahitaji ya kimsingi kama sembe na sukuma. Siki anatoa mfano wa kitoto kidogo kilichomfia mkononi mwake kwa njaa na ugojwa. Watu wengine wanakufa kwa kula mizizi na matunda mwitu. Meya anampinga Siki akidai kuwa uongozi wake ni bora na ni watu hao hao waliomchagua mara tatu, na hata akataka achaguliwe mara nne, tano na sita bado watampa kura.

Mara tu Gedi anaingia, mbio anasimama wima na kupiga saluti. Meya anamuamuru amtumie habari mhazili wake amtafute mara moja kinara wa uhusiano mwema na mawasiliano amwambie Meya anataka idhaa ya Baraza kucheza nyimbo za uzalendo kabla na baada ya vipindi maarufu.

Meya ana imani kuwa si lazima watu kushiba, maadamu nyongo zao zimeridhika. Siki hakubaliani na jambo hili. Kwake yeye, watu wenye matumbo yasiyotulia huwa akili zao nazo hazitulii na haoni haja ya kuwachezea watu nyimbo za kizalendo miaka

hamsini baada ya uhuru, kwani babu zao hawakupigania uhuru ili waje kusaliti juhudi na ndoto zao.

Siki anasisitiza kuwa watu wanakufa hospitalini kwa kuwa wanahitajika kulipia ilhali hata chakula wanachokila ni cha kuokota. Wanajidai kuwatibu watu ilhali dawa hamna na hata zikawepo hawawezi kuzimudu; ilhali afya bora na ya bure kwa kila mwananchi ni moja kati ya malengo ya mji katika mpango wake wa maendeleo ya miaka kumi. Siki anadai kuwa akina Meya hawajali chochote kuhusu watu waliowachagua, wanajifikiria tu.

Meya anakasirishwa na anayosema Siki na kumuita mtundu. Anashikilia kuwa anayosema Siki ni matusi kwake. Meya anaudhika na kumwamrisha Gedi amwondoe Siki hapo kwake mara moja na ahakikishe kuwa halikaribii lango kuu tena. Meya anamtuma Gedi kuwasiliana na mhazili wake amwambie amuandalie mkutano wa dharura ofisini na wanakamati wote wa kamati ya Meya wawepo.

Onyesho III

Ofisini mwa Meya, madiwani watatu wakimsubiri Meya. Wa kwanza ni kinara wa masuala ya usalama. Wa pili ni kinara wa uhusiano mwema, na wa tatu ni kinara wa uchumi na kazi. Diwani 1 na II wanaonekana wakimtetea na kukubaliana na Meya katika kila jambo ilhali Diwani III anaonekana akiwapinga na kutetea haki ya watu wa Cheneo. Anasema kuwa wanahitaji kujifaa kwa kuwafaa watu wa Cheneo. Anasema kuwa wanahitaji kujifaa kwa kuwafaa watu waliowachagua na wala si kufurahisha Meya kwa kuwapiga vita. Wasikilize vilio vya watu na wajue ni kwa nini wanatoa vilio hivyo.

Meya anapoingia ofisini anaanza kwa kudai kuwa baadhi ya madiwani na daktari wanawachochea watu kuwa Baraza limeshindwa kutimiza majukumu yake. Diwani 1 na II wanamuunga mkono huku Diwani III akimuuliza ikiwa ana uhakika kuhusiana na mambo hayo au amepata fununu tu.

Diwani I na II wanadai kuwa vitengo vyao havina tatizo lolote. Diwani I anatoa maoni kuwa vijana wanahitaji kutafutiwa jambo la kuuamsha uzalendo wao, kama ndugu uhusiano mwema kuandaa tamasha ambapo vijana watashindania zawadi kwa kubuni, kutunga na kucheza nyimbo zao. Kisha watafurahi na kutunukiwa zawadi ndogondogo na kuonyeshwa katika vyombo vya habari. Diwani II anasema kuwa atahakikisha mashindano yote yanaonyeshwa moja kwa moja kupitia vyombo vya habari huku uzalendo utamiminikia watu katika pembe zote za Cheneo.

Diwani III anapinga haya akisema kuwa uzalendo hauji kwa watu kuimbiwa nyimbo bali kwa kujibu vilio vyao. Diwani III anasema kuwa hauoni mpango wa kunufaisha watu kwamba wengi hawana ajira, na walio nayo mishahara yao haitoshi wala hailipwi kwa wakati. Watu wana njaa na uhitaji wa dawa ambazo kuagizwa kwake bado lakini wanazidi kuwaeleza kuwa karibuni zitawasili. Mawazo ya Diwani III yanamkasirisha Meya ambaye anaungwa mkono na Diwani I na II wakimpinga Diwani III.

Meya anatoa agizo kuwa madiwani wasitozwe kodi, na kuanzia mwezi huo mishahara yao isitozwe kodi. Diwani I na II wanamuunga mkono ilhali Diwani III akidai kuwa Baraza lina nakisi ya kutowatoza madiwani kodi ni kuongeza nakisi ya Baraza. Lakini Meya anamwamrisha Diwani III kwamba ni uamuzi wa Baraza na kuwa ile ni demokrasia. Diwani III anakubali shingo upande. Diwani I, III na Meya wanafurahia jambo hili na kupokeza mikono kila mmoja wao wakitabasamu lakini Diwani III hafurahii kamwe.

SEHEMU II

Onyesho 1

Onyesho linaanza Meya akiwa ofisini mwake kupanga mikakati ya mapokezi ya mameya kutoka nchi za nje. Anapanga kuwapa mapokezi ya kupigiwa mfano. Hoteli ya kifahari, vyakula kutoka kila utamaduni duniani, na mvinyo atauagiza kutoka Ufaransa, ili wale wa kunywa wajue kuwa Cheneo si mji hivihivi. Wajue kuwa ufadhili wao kwa Baraza unathaminiwa.

Mara Bili anaingia. Mkewe Meya amesafiri kwenda ng'ambo kuwaona watoto wake ambao wanasomea huko 'kwa sababu Cheneo viwango vya elimu viko chini'. Meya anaeleza kuwa elimu ya hapa ni ya kawaida mno na haina kubwa la kumfaa mtoto mwenye mzazi anayeona mbali. Aliko mkewe ndiko kuna wakunga wenyewe. Meya hataki kubahatisha na madaktari wa Cheneo. Vilevile mtoto atakapozaliwa atapata uraia wa huko huko. Bili anaposema kuwa Meya ana pesa licha ya hali ngumu, Meya anakubali akisema kuwa asipokuwa nazo ni nani atakuwa nazo? Ameuza vipande vyake vitatu vya ardhi kupata pesa kwa ajili hii. Amebakiza vitano '*in case*.'

Wanajadiliana kuhusu mwanakandarasi aliyepewa kandarasi na Meya mtangulizi wake. Mwanakandarsi anataka kuendelea kuleta bidhaa kwani ana mkataba unaokwisha miaka mitatu kutoka sasa, na ameenda kortini. Anadai Meya hakufuata kanuni zinazostahili kabla ya kuchukua hatua.

Bili anamshauri amwite mwanakandarasi amwambie aende kortini ambako korti itaamuru alipwe hela thamani ya pato ambalo angalipata kipindi chote cha mkataba. Ingawa Meya anawaza kuwa itabidi Baraza limlipe na Meya kuharibiwa jina, Bili anamwambia kuwa jina si kitu; tumbo lake na jamaa zake, watoto wake, wajukuu zake. Isitoshe hela atakazolipwa ni za Baraza wala si zake. Meya anafurahia ushauri wa Bili, naye Bili anamtahadharisha kuwa asimsahau.

Punde tu sauti za watu wanaodai kutendea haki zinasikika kutoka nje. Mara moja hiyo, Meya ameamini ni uchochezi wake Siki. Lakini Bili anamwambia kuwa sauti ni sauti tu! Wasemao mchana usiku watalala. Gedi anabisha mlango, anaingia na kumwambia Meya kuwa wafanyikazi wa Baraza la Jiji wamegoma, wanataka mishahara zaidi, dawa hospitalini, wanadai kumwona Meya, wanadai takriban kila kitu. Meya anamtuma Gedi kuwaambia kuwa atawafuta kazi kwani kuna vijana wengi huko nje waliohitimu kutoka vyuo vikuu ambao wameshindwa kupata hata utopasi. Meya anamtuma Gedi amwambie '*chief security*' awaite polisi.

Wanaingia wanahabari ambao wanataka kumhoji Meya kuhusu mgomo lakini Meya anamwambia Gedi awwambie kuwa yeye yuko mkutanoni. Bili anamkumbusha Meya kuwa mhubiri anaamuunga mkono, naye Meya anamwambia anahitaji maombi yake. Bili anaenda kumtafuta mwombaji.

Onyesho II

Siki akiwa ofisini kwake anapokea simu kutoka kwa Tatu. Anamwita Tatu ofisini kwake. Baada ya kuongea kwenye simu anazungumza pekee yake kuhusu hali ya watu wa Cheneo, mara Waridi anaingia mbio. Waridi anamjulisha kuwa anaacha kazi. Analalamikia hali ilivyo ofisini – wagojwa kufa ovyo, mshahara haulipwi kwa wakati ufaao, hospitali ni chafu kwani hakuna maji ya kutosha.

Kando na hayo, amepata habari kuwa huenda pakawepo migomo na maandamano siku yoyote. Siki anajaribu kumtuliza na kumshauri kuwa hali itabadilika na mshahara utakuja.

Tatu anawasili pale ofisini. Anasema kuwa kusudi lake la kufika pale ni kupata kauli ya daktari kuhusu ukosefu wa dawa hospitalini.

Kwa hivyo anaonelea washinikize Baraza la mji kuwapa watu dawa hata kama itakuwa ni kwa mkopo. Analalamika kuwa wamejaribu kutaka kukutana na Meya lakini hadi sasa hawajafanikiwa.

Tatu anapendekeza wagome lakini Siki anamuonya kuwa mgomo una madhara yake; baadhi waaweza kufutwa kazi au kama nalo Baraza la Mji litashikilia msimamo wake, watu hawatapata mishahara kwa muda zaidi, ilhali tayari wafanyikazi wanateseka. Hata hivyo Siki anakubali kumwona Bwana Fedha na Kazi za Barasa la Mji ili amweleze tena kuhusu tatizo la dawa, ili amweleze Meya. Siki anapendekezea Tatu wazidi kushinikiza kumwona Meya.

Wanapanga kutumia Kongomano la Mameya kutoka miji mingine kama nafasi nzuri ya kumshinikiza Meya kukutana nao.

Onyesho III

Mhubiri anaitika wito na kwenda kumtembelea Meya katika ofisi yake. Meya anampokea kwa moyo mkunjufu na kwa maneno matamu. Mhubiri anaombea uongozi wa Meya udumu milele. Wanapoomba, sauti zao zinapanda kiasi cha kuwafanya askari wawili na Gedi kuingia ofisini. Askari wanawaamuru walale chini na kubeba mikono juu. Wanadhani wamevamiwa lakini wanagundua ilikuwa tu ni sala. Meya anamwambia mhuburi ya kwamba Baraza la mji linaomba awe akifika mle kuliombea mara moja kila wiki. Baraza litagharamia usafiri wake na kutoa sadaka ya shilingi laki moja kila mwezi.

Onyesho IV

Matukio yanatokea nyumbani kwake Diwani III. Diwani na Siki wako barazani wanaburudika. Siki anaungama kwamba hana mkabala mwema na Meya kwa sababu Sosi hataki kuyachukulia mambo yalivyo. Siki anawapokea wagojwa hospitalini lakini hana njia yoyote ya kuwasaidia. Hakuna madawa na zikiwepo wananchi hawawezi kuzigharamia. Siki anamuomba Diwani III na 3 akamshawishi Meya ili hali hii ibadilike.

Diwani anamweleza kwamba amewahi kusema naye na hapo awali alitilia mashauri yake maanani lakini kwa sasa sivyo tena. Siki anamhiza amkumbushe tena na tena. Diwani anamweleza ya kwamba Meya anawashauri anaowategemea ingawa wanampotosha. Anaorodhesha matatizo yanayowakumba wakazi wa Cheneo kama kutwaliwa na askari wenye kutetea haki zao. Wafanyakazi wa Baraza wanafurushwa. Hana njia ya kuwasaidia wafanyakazi, ndio maana ameamua kukaa kando na kufuatilia matokeo yanavyojiri. Siki anashangaa ni vipi Meya ambaye ni mtu mmoja amewashinda madiwani wengi kumshauri.

Diwani anamweleza njaa na tama zimewapofusha madiwani, kwa hivyo wanafanya yatakayowafaidi na siyo wananchi wanaowawakilisha. Diwani anamfananisha Meya na ndovu na kwa hivyo hawezi kushindana naye kwani ana uwezo mkubwa. Anatoa

mfano wa 'Mayor's Act' inayompa mamlaka ya kuchukulia mtu hatua kali. Ya pili ni 'Riot Act' ambayo inamwezesha kuandama yeyote wakati alasiri iingiapo. Kuna sheria inayoitwa 'collective responsibility' inayomnyima mwananchi uhuru wa kwenda kinyume cha jambo hata kama halina umuhimu maadamu wengi wameliunga mkono.

Diwani anajitetea kwamba ni wananchi waliowapa cheo na itabidi waridhike na huduma wanayoitoa ingawa haistahili. Diwani anakata kauli kuwa upandacho ndicho uvunacho. Siki anapata kuelewa jinsi viongozo wao hawajawajibika.

Diwani anajaribu kumshawishi Siki aingilie siasa ili kubadilisha hali ilivyo lakini Siki anachelea kuwa siasa ni mchezo mchafu. Diwani anaungama watu wengi wanatazama kando mambo yanapoharibika kwa vile wanajinufaisha na hawaoni haja ya kufanya marekebisho. Anamuahidi Siki atazidi kumsemeza Meya kwa niaba ya wananchi. Siku ifuatayo amepangiwa kuwa na mikutano na Meya. Kuna wageni wanaotazamiwa kuja kuzuru mji.

Analalamika mji ni mchafu, unavunda na anaona haya kuwapokea wageni katika hali hiyo. Badala ya kuwasikiliza wafanyakazi na kuyakabili matatizo yao kwa njia ya wazi, Meya yumo katika harakati za kujipatia vipande vya ardhi na wenzake. Anatumia cheo chake kujilimbikizia mali. Anafananisha ile harufu mbaya ya taka iliyoghubika mji na uozo ulio ndani. Kwa mtazamo wake viongozi ni picha ya umma uliomchagua. Kama viongozi ni fisadi, umma lazima unaendeleza tabia hiyo. Itahitaji bidii maradufu ili kuung;oa uozo uliopo.

SEHEMU III

<u>Onyesho I</u>

Ni siku inayofuata, asubuhi, katika ofisi ya Meya. Diwani III amefika kwa mwaliko wa Meya. Meya anataka mishahara ya madiwani iongezwe na nyongeza hiyo mpya iwekwe katika malipo ya mwezi uo huo. Diwani III anasita kwani mishahara imeisha

kuandaliwa na pia hapakuwa na kikao cha kuidhinisha nyongeza hiyo kwa mujibu wa kanuni za Barasa. Meya anamweleza asijishughulishe na hayo.

Diwani III anamjulisha Meya kuwa wafanyakazi wamegoma kwa kuwa wanataka nyongeza ya mishahara na anabashiri iwapo mishahara ya madiwani itaongezwa, mgogoro baina ya madiwani na wafanyakazi utakolea. Meya anashikilia kuwa madiwani si wananchi wa kawaida hivyo wasilinganishwe na wafanyakazi.

Mgomo ule unaathiri pato la Baraza na hata hiyo nyongeza itakuwa vigumu kuigharamia. Meya anapendekeza wafanyakazi wasilipwe kwa zile siku walizogoma. Ana hakika mahitaji ya kila siku yatawalazimu kurudi kazini, na hali itarejea ilivyokuwa awali.

Diwani III anamkosoa kwamba Barasa na wafanyakazi wanategemeana. Hakuna mtwana. Anapendekeza wafanyakazi na madiwani wapate nyongeza safari moja baada ya mgomo kuisha. Inayojuzu ni kutafuta nyenzo za kuongeza pato la Baraza.

Meya anamkaripia angoje zamu yake ya umeya ili atekeleze hayo anayoyataka. Diwani anamuomba asichukulie maoni yake kwa ubaya wala hana tama ya uongozi. Madiwani wakilipiwa nyongeza inayopendekezwa hazina haitaweza kumudu gharama hiyo. Meya anamjulisha kuwa wale wageni wanaokuja watawapa mikopo itakayotumika kulipia mishahara.

Meya hajali yatayojiri baadaye. Diwani anamwonya kuwa vizazi vijavyo havitasahau mema au mabaya wanayotenda kama viongozi kwani uongozi hausahauliki. Anakubali kumtekelezea Meya atakayo ingawa shingo upande.

Onyesho II

Katika ofisi ya Meya sauti ya wafanyakazi waliogoma zinasikika. Wanahutubiwa na kiongozi wa wafanyakazi lakini mkutano wao unatibuliwa na askari wanaowafyatulia risasi. Meya anacheka akiwaza kuwa aliwaonya lakini hawakumsikiliza.

Gedi anakuja kumjulisha kwamba ana wageni. Ametembelewa na Bili, Bwana Usalama na Bwana Uhusiano Mwema. Anawapokea na kisha wanapiga gumzo kuhusu yaliyojiri. Walimjulisha Meya kuwa lile tisho la kuwafuta kazi wafanyakazi na kuwaajiri vijana linaweza kurushwa hewani.

Baada ya siku chache walidhamiria wafanyakazi wangerudi kuomba warejeshwe kazini na wakati huo Meya awape masharti. Bili anapendekeza ili kuwahadaa wale wageni Bwana Uhusiano Mwema angejaribu kushauriana na wafanyakazi.

Wanaamua kulipwa marupurupu kwa kazi hii ya 'overtime'. Wanaelewa Bwana Uchumi na Kazi hatakubali kuyaidhinisha malipo hayo, kwa hivyo wanapanga kuiuza fimbo ya Meya iliyotengenezwa kwa dhahabu.

Wanapanga njama kuhakikisha Bwana Uchumi na Kazi hapati habari hizi kamwe.

Onyesho III

Ni nyumbani kwa Meya. Dida, anafagia huku akiimba. Anaimba wimbo unaoashiria mvutano uliopo baina ya wanyonge na wenye nguvu.

SEHEMU IV

Onyesho I

Ni ofisini kwa Meya. Ni siku moja kabla ya kufika kwa Kongomano la Mameya. Meya anakutana na wawakilishi wa wafanyakazi. Medi anasema ajira wanayopokea yafaa iwawezeshe kumudu gharama ya maisha. Beka analalamika kuwa wanaofanya kazi, ingawa wamehudumu kwa miaka na mikaka, lakini hawana hazina ya maana ya kuweka. Tatu anadokeza mishahara yao ni midogo na umepita muda mrefu tangu wapate nyongeza.

Madiwani hujipa nyongeza baada ya vipindi vifupi vifupi wakisema gharama ya maisha inapanda kila uchao. Wafanyakazi wamechoshwa na kucheleweshwa kwa mishahara yao ilhali wakubwa wao wanapata mshahara huo. Medi anaeleza kwa

kutojali masilahi ya watoto wao hawawezi kuishi maisha mazuri. Anaona madiwani hawawezi kukubali kuwa wafanyakazi pia ni wanadamu.

Beka anataja kisa cha mtoto wake Rekecha aliyeaga kwa kukosa dawa. Kinaya ni kwamba madiwani wana bima ya matibabu katika hospitali kubwa kubwa. Pesa za kununulia chakula hazitoshi kwa hivyo hawawezi kugharamia matibabu. Meya anajitetea kwamba Baraza ni miongoni mwa waajiri wanaowalipa wafanyakazi wao vizuri. Tatu anaonyesha tofauti iliyoko katika hali ya maisha ya madiwani na wafanyakazi.

Meya anapinga kwamba hakuna tofauti kwani wanagawana pato la Baraza. Medi na Beka wanamwambia kwamba mgao huo sio sawa. Meya anawaambia wasubiri wamalize shughuli za kupokea wageni ndipo washughulikiwe. Medi anashikilia kuwa wameshasubiri na umefika wakati wa kuondoa utumwa wa siku nyingi. Tatu anamwomba Bwana Meya awape jawabu la kuwapa wenzao wanaowasubiri. Meya anashikilia kauli kuwa hakuna pesa.

Medi anauliza zitokako pesa za kuongeza madiwani. Tatu anapendekeza washirikishwe katika kikao cha madiwani ili watetee haki zao. Meya anakataa akisisitiza kwamba kanuni za Baraza hazimkubalii kuwashirikisha katika kikao hasa wafanyakazi waliogoma. Anaweza kuzungumza na wafanyakazi wakirejea kazini. Tatu anamjulisha Meya kuwa mgomo utaendelea, na mji utaendelea kuchafuka hadi watakaposikizwa.

Onyesho II

Ofisini mwa Meya, siku moja imepita tangu Meya akutane na mwakilishi na wafanyakazi. Meya analalamika kwamba wageni wanatazamiwa kuwasili siku hiyo na wafanyakazi bado wamegoma. Licha ya kukutana nao kwa mara ya pili siku hiyo, wafanyakazi walikataa kubadili nia. Diwani I anashauri wapeperushe matangazo katika vyombo vya habari kuwatangazia vijana wasio na ajira waisafishe miji. Diwani II anashauri suluhu inaweza kupatikana iwapo hali ya utulivu itakuwepo. Kwa sasa

umma ulikua umeshafahamishwa kuhusu mgomo, na Meya alihofia hangeitikia mwito. Anaanza kung'amua Diwani I na II walimdanganya. Anajuta laity angelimsikiliza Bwana Uchumi na kazi hangekuwa katika hali hii. Anapomuulizia Bili anaelezwa hajaonekana wala hapokei simu.

Wakiwa wanawaza kuhusu la kufanya Gedi anaingia mbio na kuwajulisha habari zimefika kwamba wafanyakazi wa uwanja wa ndege pia wamegoma. Ndege iliyowabeba wageni haiwezi kutua uwanjani kwani waelekezi hawapo kazini kwa kuwa wamegoma pia. Badala yake ndege zinaelekezwa kutua kwa mji. Kuna madai kuwa wageni wanaogopa mkurupuko wa kipindupindu maana mji mzima hauna maji safi.

Usafiri umetatizwa kwani wafanyakazi katika bohari la mafuta waliogoma wamefanya vituo vya kuuza mafuta visiweze kuendesha shughuli zao. Askari I na II wanaingia na kumjulisha kuwa Meya wametumwa na makao makuu kuwachukua waende kueleza mbele hali hii ya mambo. Wote wanapigwa na mshtuko mkubwa kiasi cha Meya kuzirai na kuanguka kutoka kitini.

Dhamira ya Mwandishi

Dhamira katika fasihi ni istilahi inayotumiwa kueleza wazo kuu katika hadithi au riwaya, tamthilia, hadithi fupi au shairi. Wazo hilo kuu hufungamana na lengo la mwandishi wa kazi hiyo. Dhamira pia ni dhana inayotumiwa kueleza lengo kuu la utunzi wa kazi husika. Ni suala ambalo mwandishi hulikuza na kuliendeleza sambamba na msuko na hadithi yake pamoja na mahusiano ya wahusika mbalimbali. Kwa hivyo tunapozungumzia maudhui ya kazi ya fasihi, dhamira pia hujumlishwa mumo humo.

Kwa hivyo, katika tamthilia ya Mstahiki Meya, tunaweza kusema kwamba mwandishi alidhamiria kuzungumzia masuala yafuatayo:

- Kuonyesha kuwa uongozi mbaya hudidimiza maendeleo.
- Kuwaonyesha viongozi umuhimu wa kupima ushauri wanaopewa kwani kuna ushauri mzuri na wa kupotosha.
- Ukosefu wa hali husababisha mapinduzi.

SURA YA TATU

MAUDHUI MUHIMU NA DHAMIRA

Maudhui kwa upande mwingine ni jumla ya mambo yote yanayozungumziwa katika kazi ya fasihi. Jinsi ambavyo tumetaja kuwa dhamira hufumbata maudhui, nayo maudhui hujumlisha dhamira, falsafa, itikadi na msimamo wa mwandishi. Maudhui mbalimbali yanayobainika katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* ni pamoja na:

(i)	Uongozi mbaya	(x)	Udhalimu/unyanyasaji
(ii)	Umaskini	(xi)	Ukoloni mamboleo
iii)	Nafasi ya sheria	(xii)	Haki
(iv)	Ufisadi	(xiii)	Uwajibikaji na mapuuza
(v)	Ubinafsi na umangimeza	(xiv)	Ukombozi
(vi)	Unafiki	(xv)	Huduma za kijamii
(vii)	Ubadhirifu, - anasa, starehe	(xvi)	Utabaka
(viii)	Ubarakala/ukaragosi	(xvii)	Utu na uadilifu
(ix)	Matatizo ya uchumi	(xviii)	Usaliti

(i) <u>Uongozi mbaya</u>

Uongozi mbaya ni hali ambapo aghalabu kiongozi anatumia mamlaka yake visivyo kwa kujinufaisha na kunufaisha vibaraka wake badala ya kuwatumikia raia wan chi au

eneo husika kwa kuendeleza sera potovu na hata kutozingatia sheria za nchi. Viongozi wanaotekeleza sera za kiutawala zinazokandamiza au kurudisha nyuma maendeleo ya watawaliwa huwa ni viongozi wabaya. Maudhui mengi katika tamthilia hii yamejitokeza kutokana na maudhui makuu ya uongozi mbaya. Maudhui ya uongozi mbaya yamejitokeza katika tamthilia hii ya Mstahiki Meya pakubwa.

- Uongozi mbaya unadhihirika pale tunapokumbana na kudorora kwa huduma za umma ambazo zinasimamiwa na Meya Sosi. Hizi ni kama ukosefu wa dawa au matibabu ya kuridhisha zahanatini, mfumo duni wa elimu, uchafu wa mazingira, ukosefu na uchafuzi wa maji kiasi ya kwamba hata Meya hayanywi maji hayo na mengineyo.

- Meya Sosi anasawiri uongozi mbaya hasa tunapomwona amezingirwa na vibarakala ambao hawamwelekezi ipasavyo au kumkosoa ila wanamshangilia huku Meya huyo akiwatumia kutoa maamuzi ambayo hayasaidii raia. Maamuzi haya yanamfaidi Meya mwenyewe na vikaragosi wake. Mfano ni pale Meya Sosi anapozingirwa na Diwani1, Diwani II na Bili ambao wanampotosha kwa ushauri wao na kumtumbukiza kwenye shimo.

- Uongozi wa Baraza la Cheneo unaoongozwa na Meya Sosi ni mbaya kwa kuwa unapalilia ufisadi. Meya Sosi anatumia mamlaka yake kunyakua ardhi ya umma, kuwaongeza mshahara wafuasi wake kiholela. Kuwapa marupurupu na kuwaajiri watu kazi bila kuzingatia ufaafu wao bali kwa kuzingatia mapendeleo ya kifisadi.

- Usugu wa viongozi wa Cheneo hasa Meya Sosi kuvunja sheria bila kuhofia adhabu yoyote ni dhihirisho la uongozi mbaya. Licha ya kuwa Meya Sosi amefilisi barasa la Cheneo, anamzungumzia Daktari Siki kwa ujeuri na kusuma kuwa raia wangemchagua hata mara nne akitaka kwa kuwa tayari walikuwa wamemchagua mara mbili.

- Uongozi mbaya pia unaonekana katika baraza la Cheneo pale tunaona ule ukatili na unyama unaotendewa raia hao. Wanayimwa haki yao ya kugoma wakipigania nyongeza ya mishahara na kutuma polisi wawatawanye na hata kuwaua.

- Utawala wa Cheneo chini ya Meya unavunja kanuni za Baraza hasa pale anapokataa kuzizingatia na badala yake kusikiza Bili na ushauri wake kuhusu utoaji wa kandarasi za Baraza.

- Ukosefu wa sera mwafaka na utaratibu wa kutatua matatizo – ukosefu wa dawa ni dhihirisho kuwa hakuna mikakati madhubuti ya kuhakikisha hali kama hizi zinashughulikiwa.

- Mishahara ya wafanyakazi wa Baraza kucheleweshwa na vilevile kulipwa nusunusu (uk. 23).

- Licha ya kuwa baadhi ya madiwani wanasema uchumi wan chi umeimarika lakini haumnufaishi mwananchi wa kawaida (uk. 23).

(ii) <u>Umaskini</u>

Umaskini ni hali ya kukosa mapato ya kutosha na ya kukidhi mahitaji ya kimaisha. Mtu akisemekana ni maskini huwa ana umaskini, ufukara, afakiri au yeye ni kabwela kwa hivyo ni kinyume na utajiri.

- Wagojwa wanaofika zahanatini hawana pesa za kulipia huduma wanazohitaji. Siki asema "*hawa watu hawana pesa*" (uk.2)

- Wagojwa wengine hata karatasi ya kunakilia udodosi wao hawana (uk.3)

- Wafanyakazi kama mama mwenye mtoto mgojwa zahanatini anasema amemlisha mtoto kiporo cha makombo aliyotoa kwa Mstahiki Meya. Asema chakula hicho kilikuwa kidogo hivyo yeye hakukila (uk. 4).

- Mama anapoulizwa na daktari iwapo alikitokosa chakula anasema hakuweza kwa sababu bei ya makaa na mafuta ya taa imepanda mno.

- Wafanyakazi wa Mstahiki Meya hula chakula kilichopimiwa mbwa nao hukila wasidhurike (uk.5).

- Waridi anazungumzia umaskini wan chi (uk.3) anaposema, '…… nchi yenyewe maskini; ombaomba'.

- Watoto wana utapia mlo, umaskini unawakosesha watu lishe bora. Nesi anasema; '*Kitoto chenyewe kiriba chaongoza*' (uk. 5-6).

- Nesi ni mkali (uk.3) na anawazungumzia wagojwa kwa dharau lakini umaskini unawafanya kumsihi ili angalau wahudumiwe kwenye zahanati hiyo kwa sababu hawana namna.

- Umaskini wa nchi unadhihirika katika utegemezi wa mikopo kutoka nchi geni.

- Wengi wa wakazi wa Cheneo ni maskini kiasi kwamba hawawezi kujikimu kwa chakula cha bei ya chini kama sukuma na dona. Hawawezi kugharamia elimu, aidha wanaishi mabandani. Medi anasema watoto wao anakula vya kuokota! (uk.61).

(iii) <u>Nafasi ya sheria</u>

Sheria katika tamthilia hii imetumika kuwalinda viongozi na kuwadhulumu watawaliwa.

- Uk. 3: Waridi azungumzia sheria iliyotolewa na wakubwa kuhusu kugawana gharama – kwamba wanaotafuta huduma ya afya walipie huduma hizo.

- Uk. 5: Sheria ya misitu kushika kasi – imefanya bei ya makaa kupanda.

- Katika malengo ya mpango wa maendeleo katika muda wa miaka kumi na malengo ya milenia.

- Uk. 29: Meya asema atafungwa miaka saba akipatwa na kosa kuhusu kuvunja makataa ya kandarasi.

- Kuna sheria dhalimu ambazo zinaweza kutumiwa kuwakandamiza wana Cheneo, kwa mfano uk.48: *Mayor's Act, Riot Act*. Uk.49; *Collective Responsibility*.

(iv) <u>Udhalimu/Unyanyasaji</u>

Dhulumu au udhalimu ni hali ya maonevu kwa mhusika Fulani ambapo huwa mtu ananyimwa haki yake au kunyanyaswa na mwingine au kudhalilishwa.

- Nesi hawahurumii watu wanaokuja kutafuta huduma zahanatini, kwa mfano, kwa ukali anakataa kumruhusu mama aliyekuwa na mtoto mgojwa sana kumwona daktari kwa dharura. (uk.3)

- Meya anapomfokea Dida, ijapokuwa kijakazi huyu anaomba msamaha Meya anamkea akimwambia hadithi zake za pole hazina maana. (uk.9).

- Mwenye kuyaleta mayai – mradi wake unakatizwa kwa kosa ambalo si lake moja kwa moja.

- Meya na vikaragosi wake wanaamua kuwa wafanyakazi wanaogoma watafutwa kazi bila kusikizwa. (uk.21).

- Vijana waliohitimu vyuo vikuu lakini hawana ajira wanatumiwa vibaya kwa kupendekeza kuwa wafanye kazi za waliogoma. Hana mpango wowote wa kuwasaidia vijana ndiposa anaona ni wazo zuri vijana wahusishwe kwa tamasha za nyimbo kwani watafurahia zawadi ndogo ndogo na kuonyeshwa katika vyombo vya habari. (uk. 20).

- Waliogoma waliuawa kiholela ndiposa Meya akasema wakati huo hakutaka vifo kwani wakati wa kura umekaribia.

- Madiwani wanaondolewa kodi ilhali watu wa kawaida kama muuza ndizi analipa kodi. Meya anapoulizwa kwa nini iwe hivi anadai ni uamuzi wa Baraza.

- Baraza kutarajiwa kuwapa madiwani pesa za mavazi mazuri na kuongezwa mishahara ilhali watu wafa njaa.

- Meya na Diwani I na II huwazima watu wanaojaribu kulalamikia hali duni kikazi kwa kukohoa tu (uk.16). Hili linaonyesha viongozi wanawakandamiza mno watawaliwa.

- Ushauri wa Bili, Diwani I na II kwa Meya unachangia dhuluma ambazo Meya anaendeleza kwa wana Cheneo.

- Udhibiti wa kupita kiasi ni udhalimu. Meya ndiye aliyekuwa na ushawishi mkubwa. Kile alichoamua kilitekelezwa na kiliathiri wana Cheneo. Kwa mfano, uk.59, Diwani 1 asema; *Mstahiki Meya ndiye awezaye kuchemua na wote wakapata mafua. Hawawezi kuchemua wewe upate mafua. Hata kidogo*!'.

- Sheria dhalimu zinampa nguvu Meya hivyo haikuwa rahisi kwa wana Cheneo kumpinga. Diwani III anatuelezea kuhusu *Mayor's Act*, *Riot Act* na suala la *Collective Responsibility*. *Mayor's Act*, kwa mfano, '….. inatosha kumkunja kila aliye chini yake kama ua wakati wa alasiri', (uk.49).

(v) <u>Ubinafsi na Umangimeza</u>

Ubinafsi ni ile hali ya kujitakia mema wewe pekee yako bila kujali maslahi ya wenzako au hata kufanyia wenzako maovu ili ujinufaishe mwenyewe. Isitoshe, ubinafsi unaelezea dhana ya kuwa mhusika anajipenda mwenyewe na huona ulimwengu ukimzingira yeye pekee yake bila kuwafikira wenzake. Umangimeza nao unaweza kuelezewa kama hali ya mtu kuwa na tama inayokithiri mipaka ya kuhodhi na kujilimbikizia mali au utajiri na huwa mhusika haridhiki na kiwango chochote cha mali hiyo.

Utashi huu wa kiwendawazimu wa kujitajirisha baina ya viongozi wengi ni mojawapo wa saratani inayokeketa na kufifisha uchumi wa mataifa machanga na kuwaacha hoi wananchi wake. Rasilmali za nchi kama migodi, mafuta na mapato ya umma huliwa na viongozi walio na umangimeza. Neno hili lilipata umaarufu tangu lilipoanzwa kutumiwa na aliyekuwa rais wa Tanzania Ali Hassan Mwinyi. Hali hizi zinaadhihirika wazi kama maudhui bayana katika tamthilia hii ya *Mstahiki Meya*.

- Madiwani, kila wanapokuwa na mikutano, hujadili maslahi yao ilhali walichaguliwa kuhudumia wana Cheneo.

- Meya na madiwani wanajilimbikizia nyongesa za mishahara na marupurupu wakati ambapo wafanyakazi walikuwa wakigoma kwa kutolipwa.

- Meya na madiwani wanajiondolea mzigo wa kulipa kodi na wanawatwika mzigo huu wananchi wa kawaida, kama mama muuza ndizi.

- Zaidi ya kujiongeza mishahara na kutolipa kodi, Meya na madiwani wanaafikiana na Bili kuuza fimbo ya Meya ili kupata pesa kwa manufaa yao wenyewe.

- Meya anatamani kubaki uongozini. Ameongoza mara tatu na hayuko tayari kubanduka, kwa hivyo anatumia asasi na mbinu mbalimbali kama usalama, dini, vibaraka, vyombo vya habari na washauri wa kibinafsi ili kubaki uongozini (uk.12).

- Mhubiri anajua hali ya wana Cheneo na utawala dhalimu wa Meya lakini kwa vile anataka kunufaika kibinafsi, anatoa huduma kwa Meya na kupokea laki moja na pesa za kugharamia petrol.

- Meya na madiwani wanajipendelea katika kupata huduma, kwa mfano, wana bima ya matibabu, karo na usafiri wa watoto wao nao wana Cheneo wanaishi kwenye mabanda, watoto wanafukuzwa shuleni kwa ukosefu wa karo na wana wao wanakufa kwa njaa.

- Meya anakubali ushauri wa Bili kuhusu kukatiza kandarasi ili Baraza lishtakiwe kasha korti ikimpa fidia mwanakandarasi huyo agawane pesa hizo na Meya.

- Meya anaishinisha kwamba walinda usalama waongezewe mshahara ili kulilinda Baraza na wakati huo Cheneo ilikuwa na mahitaji mengine muhimu.

(vi) <u>Ukengeushi/Mkengeuko</u>

Kukengeuka kwa mujibu wa *Kamusi ya Karne ya 21* ni kuasi au kupotea njia. Mkengeuko kwa hivyo ni kwenda kombo na kufanya kinyume cha majukumu uliyopewa au matarajio ya jamii au kuacha njia na kufuata nyingine tofauti kabisa. Wahusika hukengeuka kimila, kikazi, kitabia n.k.

- Meya amekengeuka. Yeye kama kiongozi wa Baraza hajafanya juhudi ya kuboresha huduma za jamii kama vile elimu, matibabu, maji na usafi. Katika uk. 26, Meya anakiri; '*Elimu yetu hapa ni ya kawaida mno. Haina kubwa la kumfaa mtoto mwenye mzazi anayeona mbali*'. Bili anachangia kwa kusema elimu hiyo ni ya akina yakhe.

- Kuhusu mazingira tunaona kuwa taka hazijazolewa, kiasi cha uvundo kuingia kwenye ofisi ya Meya. Kuhusu utabibu tunaona kwamba hakuna dawa zahanatini na chache zilizoko wagojwa hawana uwezo wa kuzinunua.

- Bili anadhihirisha ukengeushi pale ambapo hampi Meya ushauri wa kweli. Anamwelekeza pabovu. Kwa mfano anampa Meya njia mbaya za kifisadi kuhusu kandarasi, uuzaji wa fimbo ya Meya na ardhi.

- Gedi anatakikana kutoa huduma ya usalama kama mlinzi, lakini anafanya kazi ya tarishi, wakati huo huo anakuwa mhazili. Kwa mfano yeye ndiye anayemletea Meya habari na hata maji.

- Mhubiri anafaa kumkemea Meya katika maovu yake badala yake anamsifu na kumwombea adumu milele. Hali hii inatilia mbolea udhalimu dhidi ya wana Cheneo.

- Mhubiri anaabudu pesa kiasi cha kumuasi Mungu. Anafurahia ile laki moja na mapeni ya petrol anayopewa na Meya na kusahau jukumu lake la kuelekeza.

- Meya akiwa kiongozi wa Cheneo anastahili kuwa mzalendo ila anataka watoto wake wapate uraia wa nchi ya kigeni (uk.27).

- Meya na Diwani I na II wamekengeuka kwani walichaguliwa na wana Cheneo ili kuendesha Baraza. Hata hivyo wanajishughulisha na maslahi yao tu katika vikao vyao vyote vya Baraza.

(vii) <u>Ukoloni Mamboleo</u>

Ukoloni mamboleo ni ile hali ya mataifa wafadhili au ya kigeni kudhihirisha ushawishi wake kwa mataifa ya ulimwengu wa tatu kwa kushurutisha uwepo wa masharti ya kiuchumi, kiasa, kijamii na hata kiteknolojia.

Ukoloni mkongwe nao ni hali ya nchi kuidhibiti au kuikalia nchi nyingine kimabavu kwa misingi ya kisiasa na kiuchumi kama wakati mataifa machanga barani Afrika yalipotawaliwa moja kwa moja na wakoloni kutoka bara Uropa. Wakoloni hapa walipoondoka na mataifa haya machanga kupata uhuru, bado wameendelea kuaathiri mataifa haya. Athari hizi hudhihirika kupitia masharti yanayowekewa mataifa haya machanga na mahusiano ya kiuchumi na kisiasa baina yao na waliowatawala. Huu ndio ukoloni mambo leo.

- Dawa inaagizwa kutoka nchi za mbali. (uk.2) shehena zasemekana ziko bahari kuu.

- Watoto wa tabaka tawala wanasomea ng'ambo na akina yakhe ndio wa kung'ang'ana na elimu inayotolewa miaka hamsini baada ya uhuru. (uk.26).

- Meya anapotahadharisha kwamba kukaidi mipango ya mataifa ya nje kuhusu malengo ya milenia ambayo ni ya wafadhili ni hatari. (uk.14).

- Siki kulalamikia hali ya kufuata ushauri wa nchi za kigeni ambao hawakushirikishwa ni ukoloni mamboleo.

- Kugawana gharama za huduma ni wazo la mataifa ya kigeni ilhali wananchi hawana uwezo kifedha. (uk.3).

- Dhana ya ubwana na utumwa inadhihirika katika mahusiano baina ya bwana Meya na wafanyakazi wake Gedi na Dida. Hii ni ishara ya ukoloni mamboleo tunaoupata katika mataifa mengi machanga miaka mingi baada ya kuondoka kwa wakoloni. Gedi kila anapoitwa na Meya anaitika '*yes Sir*'. Meya anapokosa hisani anapopewa pole na Dida katika uk. 9 inagogoteza hali hii.

- Hali ya nchi kiuchumi ingali ileile ya ombaomba miaka hamsini baada ya uhuru. Uongozi wa Baraza unawanyonya wafanyakazi namna walivyofanya wakoloni. Kwa mfano wafanyakazi wa Baraza hawalipwi mishahara, wanapolipwa ni nusunusu na wanatozwa kodi, ilhali madiwani wanajipa nyongeza na kukwepa kulipa kodi.

- Utegemezi wa mikopo kutoka nchi za kigeni kwa mambo ya kimsingi kama vile kulipa mishahara ya wafanyakazi. (uk.20).

- Hali ya kupewa ufadhili kwa masharti, kwa mfano kupewa mkopo lakini kulazimishwa kupunguza idadi ya wafanyakazi. (uk.20).

(viii) <u>Matatizo ya Kiuchumi</u>

Uchumi ni yale mapato yatokanayo na shughuli za watu nchini na matumizi ya mapato hayo. Uchumi pia ni hali za uzalishaji mali na jinsi mali hiyo inavyoenezwa kwa raia katika nchi hiyo.

- Beka anazungumzia mfumko wa bei anapomlalamikia Meya kuhusu matatizo ya wafanyakazi. (uk.68)

- Gharama ya maisha kupanda, mahitaji yanaongezeka ilhali mshahara ni ule ule haupandi. (uk.11)

- Kuna ukosefu wa chakula na maji. Tunaelezwa kuwa sembe na sukuma vinawatoa watu jasho kuvitia mezani. Watu wanakufa kwa njaa. (Uk.11)

- Migomo ya wafanyakazi wa Baraza na katika uwanja wa ndege ni ishara ya matatizo ya kiuchumi.

- Wafanyakazi kujiuzulu kwa sababu walikuwa hawajapewa mshahara na wengine kulipwa nusu kwa mfano Nesi.

- Ukosefu wa dawa zahanatini unaashiria hali duni ya kiuchumi Cheneo.

- Utegemezi kwa mikopo ili kulipa mishahara na mahitaji mengine ya watu wa Cheneo kama vile chakula na njaa. Uk. 20-21.

- Masharti ya nchi fadhili zinazorejelewa katika uk. 20 kama '*kaka zetu*' yanaathiri uchumi wa Baraza la Cheneo kwa kuwa hata wanawalazimisha kupunguza idadi ya wafanyakazi. Aidha inasemekana wafadhili hawa hawajatoa ufadhili wa mkopo na hivyo baraza haliwezi kuongeza watu mishahara, kuwalisha wala kugharamia matibabu (uk.20-21). Hii ni hali halisi ya mahusiano katika mataifa fadhili na nchi changa.

- Uongozi wa Baraza unatoa elimu isiyoelekea kukidhi mahitaji ya watu wake. Ndiposa wanaofuzu vyuo vikuu hawapati hata utopasi, hivyo hawachangii katika uzalishaji mali Cheneo kwa kutumia ile nguvu kazi ilionaswa vyuoni. (uk. 20)

- Baraza la Cheneo lina nakisi ya milioni mia ishirini.

- Kwa mujibu wa Diwani III uchumi bado haujaimarika kumfaidi mwananchi wa kawaida. (uk.23).

(ix) <u>Ubadhirifu</u>

Ubadhirifu ni hali ya kuavya, kufuja au kutumia mali au rasilmali ya nchi kwa njia ya kianasa bila uangalifu au kwa njia ya kuharibu. Ubadhirifu umejitokeza mahali kwingi kwenye tamthilia hii.

- Nyumbani kwa Meya kuna vyakula vya kila nui. Mbali na mayai na chai, kuna vyakula vya aina mbalimbali mezani. (uk.8).

- Maandalizi ya takrima kwa wageni watarajiwa yalikuwa ya gharama ya juu. Kulikuwa na mipango ya kuwapa wageni watarajiwa 'makaribisho ya kupigiwa mfano – Hoteli ya kifahari, vyakula vya tamaduni zote duniani, mvinyo wa Urusi wa divai ua Ufaransa, wajue Cheneo na mji wa kutajika, waone ukarimu na udugu wetu!!!'. (uk.25).

- Kuna ubadhirifu kwenye kiasi cha sadaka ya shilingi laki moja inayotolewa kwa mhubiri kila mwezi na kugharamia petrol ya kumleta mhubiri kwa Meya na kumrudisha. (uk.44).

- Watu wa Cheneo wafa njaa huku Meya akiwa na '*entertainment vote*' ambayo hata haitumii, inangoja ualishi tu. (uk.27).

- Madiwani kutumia rasilmali za Baraza kwa shughuli za kibinafsi ilhali wanalipwa vizuri kwa mfano watoto wao kupelekwa shule na magari ya Baraza na karo yao yalipwa na Baraza la jiji.

- Madiwani kuongezwa mshahara kiholela. (uk.52).

- Meya anapokubali kuwapa madiwani marupurupu Baraza likiwa na nakisi kubwa. (uk.61).

- Meya kukubaliana na madiwani kumlipa Bili kwa ushauri ambaye si mfanyakazi wa Baraza. (uk.61).

(x) <u>Uwajibikaji na Mapuuza</u>

Uwajibikaji ni hali ya kufanya jambo ambalo unapaswa kulifanya au pale mhusika anapotimiza majukumu yake kwa kujitolea bila kujali hali ya mambo ilivyo. Mhusika anayekwepa majukumu yake na kutowajibika huwa anasemekana kuwa ana mapuuza. Katika tamthilia ya 'Mstahiki Meya' maudhui ya uwajibikaji yamejitokeza njia mbili; maudhui yanayodhihirisha uwajibikaji nay ale ya mapuuza (kukosa kuwajibika).

a) <u>Uwajibikaji</u>

- Kuwepo kwa daktari katika zahanati isiyo na dawa.
- Kuwalaza wagojwa japo hakuna dawa ili kuwapa tumaini.
- Daktari Siki anapomshauri Nesi kumkorogea mtoto anayeendesha mchanganyiko wa sukari na chumvi kwa maji moto.
- Kuwatetea wagojwa ambao hawakuwa na pesa za kulipia huduma kulazwa.
- Amri kandamizi haikuruhusu wasio na pesa kuhudumiwa lakini Daktari Siki anawajibika ili kuokoa maisha.
- Siki alimwendea Meya kueleza hali duni ya hospitali na mahangaiko ya wana Cheneo.
- Siki anamtahadharisha Meya dhidi ya uongozi wake mbaya.
- Diwani III anawajibika kwa kumpendekezea Meya kuhusu mikakati inayolenga kuwanufaisha wana Cheneo na kusuluhisha matatizo kama vile umaskini, ukosefu wa ajira na mishahara duni.

- Diwani III anavyopinga maamuzi ya Meya na wale madiwani wengine aliyoona yanakosa maadili, kwa mfano kuongeza mshahara, marupurupu na kutotozwa kodi.

- Tatu, Beka na Medi wanawajibika wanapokwenda kwa Meya kuwakilisha malalamishi ya wafanyakazi.

b) <u>Mapuuza na Kutowajibika</u>

- Baraza kutowalipa wafanyakazi inavyostahili baada yao kutoa huduma kwa Baraza.

- Zahanati iliyofaa kutoa huduma hasa kwa wafanyikazi wa Baraza haina dawa kiasi cha watu kufa kwa ugojwa usio mkubwa.

- Meya anadhihirisha kutowajibika kwa kupuuza anapofahamishwa kuwa kuna kitoto kilimfia Daktari Siki mkononi kwa njaa na ugojwa – anauliza; '*Huyo mmoja tu?... Cheneo ina watu wangapi?...*' (uk.12). Japo ni mtoto mmoja aliyekuwa anaelezwa kumhusu maisha yake ni muhimu.

- Meya anapuuza malengo kuhusu mpango wa maendeleo kwa kipindi cha miaka kumi ambayo yangeleta mafanikio ya moja kwa moja kwa wana Cheneo. Anasema mipango hiyo ya miaka kumi ni upuuzi, japo anapendekeza malengo ya maendeleo ya milenia ambayo ni ya kijumla.

- Diwani I na II wasema jukumu lao ni kuliletea Baraza linaloongozwa na Mstahiki Meya kwa sababu walitunukiwa heshima kuwa na vinara kasha wanalipwa kufanya hivyo.

- Meya hawajibika katika kutuunza rasilmali za umma. Kwa mfano, badala ya kulinda ardhi ya umma anajigawia yeye na Bili vipande vya ardhi hiyo.

- Madiwani kama viongozi waliochaguliwa wanatelekeza majukumu yao na badala yake kujali maslahi ya Meya tu. Hawatendi kazi jinsi inavyostahili.

- Madiwani wanapewa nyadhfa kama vinara ili kutekeleza majukumu fulani kwa sababu Meya alijua uwezo wao kumfaa yeye au kujifaa wao wenyewe. Kwa mfano kianara wa masuala ya usalama na yule wa uhusiano mwema hawafanyi kazi kama inavyostahili, ndiposa kuna migomo na ukosefu wa usalama.

- Meya hawajibiki ndiposa kuna migomo na ukosefu wa usalama.

- Meya hawajibiki ndiposa taka katika barabara za mji hazijazolewa hadi harufu inafika kwenye ofisi yake. (uk.19).

- Meya hawajibiki katika kusuluhisha matatizo ya wafanyakazi. Wanapolalamika kupitia viongozi wao, anatumia mbinu mbadala za kifisadi kujaribu kuwanyamazisha viongozi hao.

- Madiwani wanapojiondolea jukumu la kulipa kodi wakati mama muuza ndizi analipa kodi. (uk.21).

- Askari kutoka makao makuu kuwashika Meya na madiwani ili kujibu mashtaka kuhusiana na hali mbaya ya Cheneo.

(xi) <u>Ufisadi</u>

Ufisadi ni kule kujipatia mali au kuwezesha hali Fulani kufaulu/kufanikiwa kwa kutumia njia za mkato na zisizo za kimaadili kama ushawishi wa hela, mapendeleo ya kinasaba/kikabila au hata msukumo wa cheo kwa minajili ya kujinufaisha. Wa aidha, ufisadi ni ulaji rushwa au matumizi ya hongo au mlungula. Ufisadi ni maudhui ambayo yamejitokeza kwingi katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*.

- Panapotokea shida Meya huunda kamati za utatuzi japo hazina umuhimu kwa Baraza la Cheneo. (uk.22 Diwani III) kamati hizi hutumiwa kudhibiti uongozi dhalimu wa Mstahiki Meya. Wanakamati hawa hulipwa kwa huduma zao.

- Pendekezo la Diwani I kuwa vijana watunukiwe zawadi na waonyeshwe katika vyombo vya habari kama fursa ya kuonyesha uzalendo wao. (uk.20). Hii ilikuwa mbinu mojawapo ya kuwasahaulisha hali duni ya maisha yao.

- Nakisi ya milioni mia moja na ishirini katika Baraza la Cheneo na Meya asema watafidia.

- Madiwani kujiondolea kodi ilhali watu wote hata muuza ndizi anatozwa kodi. (uk.22).

- Meya anapoelezwa kuhusu nakisi anasema si neno akidai kuwa anajua diwani wana njaa hivyo wasilipwe kodi.

- Meya kutaka walinzi wa Baraza waongezwe mshahara kulifaa zaidi kama hospitalini, kiwanja cha ndege na wanaozoa taka hawalipwi mshahara, wacha nyongeza.

- Meya na rafikiye Bili walinyakua mashamba wanayogawana kama njugu. (uk.27).

- Ushauri wa Bili kwa Meya alipotaka kumpokonya aliyepewa kandarasi unaashiria ufisadi. Anampendekezea Meya asikilizane na aliyepewa kandarasi kuwa waikatize kandarasi yake, halafu mtu huyo amshitaki Meya. Korti ikiamua alipwe kulingana na mkataba wa kandarasi basi mwenye kandarasi ampe Meya sehemu yake. Asemavyo, '*Dawa ya adui ni kummegea unachokula – hakudhuru tena*'. (uk.29).

- Kutofuatwa kwa sheria za kutoa kandarasi katika Baraza la Cheneo. Tayari mwenye kandarasi alikuwa ameenda kortini.

- Ushauri wa Bili kwa Meya kuwa tumbo ni muhimu kuliko jina anapomzungumzia kuhusu kuvunja sheria za kandarasi.

- Bili anapopendekeza kuwa wakili wa Baraza aendeshe kesi kuhusu ile kandarasi waliopanga kuivunja, kasha Meya akubaliane na huyo wakili kumpa fungu lake baada ya kulipwa.

- Bili rafikiye Meya humfunza Meya njia zote za ufisadi naye kufaidi, kwa mfano viwanja vya umma wanavyowagana.

- Watu wafa kwa njaa na maradhi ilhali Baraza linatoa 'sadaka' ya laki moja kwa mhubiri kila mwezi na pesa za petrol; kinaya hiki.

- Meya hula njama na Bili, Diwani I na Diwani II kuiuza fimbo ya dhahabu ya Meya kasha wagawane pesa.

- Bili hulipwa na Baraza la Jiji kwa huduma za ushauri anaotoa kwa Meya. (uk.61)

- Meya alimuajiri mhazili ambaye hakustahili kupata kazi.

- Rasilimali za Baraza kutumiwa vibaya na viongozi wa Baraza. Kwa mfano watoto wao wanachukuliwa nyumbani kupelekwa skuli kwa motokaa za Baraza, mishahara ya Meya na diwani wenzake pia iko juu sana.

- Baraza la Jiji linaendeleza ufisadi kupitia zahanati. Tunaona wagojwa waliolazwa hawapati dawa ilhali wamelipia huduma. (uk.6)

(xii) <u>Unafiki, Uwongo na Propaganda</u>

Maudhui ya unafiki, uongo na propaganda yanaweza kuwekwa pamoja kwa kuwa dhana hizi tatu zinahusiana kwa karibu sana. Unafiki ni ile hali ya mtu kujaribu kuonyesha uongofu au uadilifu wa kitabia huku yeye anatenda kinyume kabisa na hulka hiyo anayowania kuisawiri. Mtu mnafiki hujifanya kuwa ana desturi, hisia au maadili ambayo kwa kweli hana.

Unafiki ni kuishi katika ulimwengu wa uongo kwa kuwasilisha picha tofauti ya maadili yasiyokuwepo. Uongo nao ni hali ambayo si kweli. Watu wanaotumia propaganda huwa wanapanga uongo huu kiudanganyifu na kuufanya uonekane kama ni kweli.

Kwa hivyo propaganda ni uongo '*uliopaliliwa*' na kupangwa ili ukae kama ukweli. Viongozi wengi hujaribu kutumia mbinu ya propaganda ili kuwafunga macho watawaliwa. Propaganda huwasaidia watawala hawa kubakia uongozini na kuendelea kutawala huku wakijifaidi wenyewe bila kuonekana wabaya. Hali hizi zimesawiriwa katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*.

- Mstahiki Meya anadanganya daima kuwa dawa zinazohitajika kwenye zahanati zilishaagizwa na kuwa shehena ipo bahari kuu yaja. Hii ni propaganda ya kuonyesha kuwa anajali na kuwapa matumaini wagojwa.

- Meya anapotahadharishwa kuhusu kutowajali waliomchagua anasema kuwa yeye kachaguliwa na watu wake wenye mahitaji mengi, mara tatu kwa sababu anatumia akili ambayo ni mali.

- Wafanyakazi wanapewa malipo duni na aghalabu wanalipwa nusu nusu ili wazidi kuwa na matumaini daima huku wakiumia.

- Meya anapopanga na vikaragosi wake kuitoa fimbo ya Meya, kuiuza na kujinufaisha kasha wadanganye kuwa ilipotea kutokana na rabsha ya mgomo. (uk.61-62).

- Viongozi wa kamati hulipwa vizuri na wanajifanya kwamba bado ni wahitaji.

- Uongozi wa Baraza unatumia mbinu danganyifu kuonyesha hali ni nzuri na huku kuna matatizo mengi. Kwa mfano kinara wa maswala ya uhusiano bora badala ya kukabili matatizo yanayowakumba vijana na kuyatatua anatumia mbinu za kinafiki pale ambapo anapanga kuwafurahisha vijana kwa zawadi ndogo ndogo na kuonyesha ulimwengu kupitia vyombo vya habari.

- Uongozi wa baraza walijinufaisha kwa jasho la wafanyakazi, hata hivyo walidai kuwa waligawana sawa chumo la Baraza na wafanyakazi wengine. (uk.69).

- Meya anapojitia ulokole usiokuwepo anadhihirisha unafiki wa hali ya juu. (uk.41) Meya anadai mara mbili hivi karibu aache kazi yake akashirikiane na mhubiri kueneza injili.

- Mhubiri ana uhusiano wa karibu sana na Meya. Tunamuona mhubiri akija kufanya maombi na kumsifu Meya ilhali anaona na anayafahamu hali ya wafanyakazi na matatizo ya wana Cheneo. (uk.41-44).

- Mhubiri hakashifu mabaya katika uongozi wa Meya bali anamdanganya kuwa kazi yake ni nzuri na anazidi kumuombea.

- Mpango wa Meya na vikaragosi wake kuiba fimbo na kuiuza kasha wadai imepotea wakati wa rabsha zilizosababishwa na wafanyakazi wanaogoma. Hii ni njama ya uongo na unafiki ili wapate nafasi ya kuiuza na kujinufaisha.

- Meya na madiwani wake wanapotoa picha nzuri ya Baraza lao kwa mataifa ya kigeni, hali ikiwa kinyume. (uk.61,73).

- Baada ya kupanga njama kuiiba fimbo ya Meya kwa manufaa yao wote, Bili anatoweka na fimbo hiyo.

- Wakati wa mgomo Meya alichelea watu kufa kwa kupigwa na askari kwa sababu ingemchafulia jina akakosa kura. (uk.19).

- Dida anasema kuwa wafanyakazi waliogoma wanapopigwa risasi na kuuawa viongozi wanakana. (uk.65).

(xiii) utetezi wa <u>Haki</u>

Ni haki ya kila mfanyakazi kulipwa mshahara kwa kazi waliofanya kwa wakati. Mishahara ya wafanyakazi Cheneo huchelewa na wakati mwingine kulipwa nusunusu. Lakini viongozi wa Baraza wanapata mishahara yao.

Wafanyakazi wote wana haki ya kuongezwa mshahara. Lakini katika mji wa Cheneo viongozi ndio wanaojiongeza mshahara huku wafanyakazi wakigoma kwa kunyimwa haki hiyo.

Wana Cheneo wote wana haki ya kuhudumiwa zahanatini. Lakini viongozi hawajawajibika kuhakikisha kuweko kwa dawa ili wapate huduma hiyo.

Wagojwa wana haki ya kumwona daktari na kusikizwa, kinyume na Waridi anavyomfokea mama aliyeleta mwanawe mgojwa zahanatini kutibiwa. (uk.3).

Meya hawapi wafanyakazi nafasi ya kuwasilisha malalamishi yao kwa kudai kuwa '*diary*' yake imejaa. Hili linaonyesha ukosefu wa haki ya kusikizwa.

(xiv) <u>Usaliti</u>

Usaliti ni kitendo cha kumhini, kumwasi, kumgeuka au kumchongea mtu wakati anakutegemea au kukuamini. Usaliti unaweza kuonekana baina ya mtu na nchi yake au hata kusema siri za ndani kwa wengine.

Mstahiki Meya anawasaliti wana Cheneo kupitia uongozi wake kwani huduma za umma ni mbovu, kwa mfano mazingira ni machafu, zahanatini hakuna dawa, ukosefu wa maji.

Meya anawasaliti wafanyakazi kwa kutowalipa mshahara ipasavyo. Anawalipa mshahara duni na kuwacheleweshea hata kwa miezi mitatu na aghalabu ukiwa nusunusu.

- Askari wa Baraza wanawasaliti wana Cheneo. Badala ya kulinda usalama wao wanawapiga wafanyakazi kiasi cha kuwaua.

- Diwani wa I na II wanawasaliti kamati zao kama vinara. Hawakushughulikia masuala ya usalama na uhusiano mwema Cheneo badala ya kumshauri Meya ipasavyo, wanampa ushauri ambao hatimaye unaumiza wana Cheneo.

- Nesi anawasaliti wagojwa anapoacha kazi kwa sababu ya malipo duni na ukosefu wa dawa.

- Bili alimsaliti Meya kwa kumpa ushauri mbaya, kwa mfano, kuhusu kandarasi, uuzaji wa fimbo ya Meya, kujigawia vipande vya ardhi ya umma na kuumiza wanaogoma.

(xv) <u>Uzalendo</u>

Uzalendo ni hali ya kuwa na mapenzi ya dhati ya kuitumikia taifa lako na hata kujitolea mhanga kwa nchi hiyo na hata pengine kuweza kuifia.

Ukosefu wa uzalendo huwa ni usaliti. Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* kuna sehemu mbali mbali ambapo wahusika fulani wana uzalendo kwa nchi yao.

- Siki alikuwa mzalendo kwa kujali maslahi ya raia wenzake na kumkabili Meya kuhusu uongozi wake mbaya.

- Siki ana ukakamavu katika majukumu yake kwenye zahanati. Anakubali kukaa zahanatini hata ingawa hajalipwa mshahara. Hali pale zahanatini ni duni kwani hakuna dawa na anawajibika anapomwambia Nesi amkorogee mtoto mgojwa chuvi na sukari kwa maji moto.

- Diwani III anadhihirisha uzalendo kwa kupinga maamuzi mabaya wanayowafanya Meya, Diwani I na II na Bili. Anaposhinikizwa kuyatekeleza anafanya hivyo shingo upande.

- Diwani III ana mwelekeo wa kizalendo wa kuleta ufanisi Cheneo. Anasema, '*Tunahitaji … kuwafaa watu wetu; tuyafanye maeneo yote ya Cheneo kuwaka moto wa mafanikio*'. (uk.17)

- Beka, Medi na Tatu ni wazalendo kwani wanakubali kuwawakilisha wafanyakazi wenzao kama viongozi.

- Wawakilishi wa wafanyakazi wanaonyesha uzalendo kwa kutetea haki za wafanyakazi mbele ya Meya kwa ujasiri na ukakamavu. (uk.66)

(xvi) <u>Uadilifu na Utu</u>

Uadilifu ni hali ya kuongka au kutenda jambo bora au la kimaadili katika jamii hata kama kuna ushawishi wa kufanya kinyume na hilo. Ni kule kuwa na nidhamu ya kutenda lililo bora kwa msukumo wa dhamiri ya mhusika bila kujali hali zinazolizingira.

- Ingawa Meya ni binamuye, Siki hatumii nafasi hiyo kuungana na Meya katika kutenda maovu. Badala yake anamkosoa na kumwelekeza.

- Siki alikuwa na nidhamu ya kwenda kazini na kutoa huduma ijapokuwa zahanatini haikuwa na dawa.

- Siki anadhihirisha uadilifu na utu anapomshughulikia yule mama mwenye kitoto kigojwa bila kutilia maanani Nesi aliyekuwa anamfokea kuwa afuate foleni.

- Wagojwa wasio na pesa wanaruhusiwa kulazwa kutokana na ushauri wa Siki. (uk.3).

- Siki anamshauri Nesi kukoroga mchanganyiko wa sukari, chumvi na maji moto ili kuokoa maisha ya kile kitoto.

- Diwani III ana nidhamu ya kazi kwa sababu anashikilia kuwa kazi ifanywe kwa mujibu wa kanuni zilizowekwa, kwa mfano, anapinga wazo la madiwani kuongezwa mshahara na kuondolewa kodi wakati raia wa kawaida wana mshahara duni na wanalipa kodi. (uk.22-23).

- Nesi amekosa utu anapomfokea mama mwenye kitoto kigojwa.

- Meya anakosa utu anapoonyesha kutojali anapoarifiwa na Siki kuhusu kitoto kilichoaga. (uk.12).

- Wafanyakazi waliogoma wanapigwa na kuuawa na askari. (uk.19,65).

- Meya hasikizi wafanyakazi waliogoma, na badala yake kupanga kuwafuta kazi.

(xvii) <u>Utabaka</u>

Utabaka ni hali ya kijamii ambapo watu huwa wanajitenga au kutengwa katika ngazi/daraja au safu tofauti za kijamii, kiuchumi na kadhalika.

Aghalabu huwa kuna tabaka la juu kama watu walio na mali na mara nyingi huwa ndio viongozi. Tabaka la chini huwa mara nyingi ni wale maskini au wasionavyo ambao huwa pia ni watawaliwa.

- Kuna utabaka katika misingi miwili; mamlaka na elimu.

- Katika msingi wa mamlaka una vikundi viwili vya watu, watawala na watawaliwa. Watawala ndio wenye kumiliki nyenzo za kiuchumi kwa mfano wana vipande vya ardhi, wana bima za matibabu na watoto wao wanasomea shule za ng'ambo. Wanakula chakula bora (uk.8) na mishahara yao ni mikubwa na usafiri wao ni magari. Watawaliwa nao ni maskini kwa mfano tunapoelezwa kuwa watoto wao wana utapia mlo, wanakula chakula cha mbwa na pia mizizi na matunda ya mwituni. Wafanyikazi walinyimwa huduma zahanatini na walipoipata ilikuwa mbovu. Watoto wa wafanyikazi walitembea kwenda shuleni na aghalabu walifukuzwa huko kutokana na ukosefu wa karo.

- Tukizingatia elimu, kuna waliosoma. Siki na Waridi ni wasomi. Hili linadhihirika, kwa mfano, kutokana na maongezi yao ya kitabibu katika (uk.5) wanataja *food poisoining* na *pain killers*.

- Siki anasawiriwa kama msomi anapojitofautisha na Meya kitaaluma kwa kusema yeye ni daktari sio mwanasiasa.

- Diwani I wa III pia ni msomi kwani anazielewa vizuri sheria na kanuni za kazi kwa mfano, *Mayor's Act, Riot Act* na *Collective Responsibility*.

Diwani II anasema kuwa waliogoma watasukumwa hadi wajue kuwa kuna wananchi na wenyenchi. Hii ni kumaanisha kuwa kuna watu wa tabaka la juu na la chini. (uk.60).

(xviii) <u>Huduma kwa Umma</u>

Huduma kwa umma katika jamii ya Cheneo inaweza kuchukuliwa kama maudhui mojawapo katika tamthilia hii ya Mstahiki Meya.

(xix) <u>Ukaragosi na Ubarakala</u>

Ubaraka/ubarakala au ukaragosi ni hali ya kumfuata mtu mwenye ushawishi mkubwa, mamlaka au utajiri kwa kumwabudu na kukubaliana na chochote asemacho bila kumpinga au kukosoa hata akiwa makosani yakini kwa minanjili ya kunufaika kutoka kwake. Wafuasi hawa ndio huitwa vikaragosi au mabarakala, pengine vibaraka. Ukaragosi umedhihirika katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*.

Diwani I na II ni vibaraka wa Meya. Tunaona wakiunga mkono kila analosema Meya hata likiwa kosa.

(xx) <u>Dini</u>

Mhubiri ni kiwakilishi cha dini. Hata hivyo tamaa yake ya pesa inamfanya kukosa kumkemea Meya kama inavyotarajiwa.

Meya anajidai mcha Mungu ilhali vitendo vyake ni kinyume na usemi huu. (uk.41).

(xxi) Ukombozi

Ukombozi ni hali ya kutoa mtu au watu kutoka hali kandamizi na kumfanya awe huru. Harakati za ukombozi huendeshwa kwa kuwazindua wahusika waliodhulumiwa na hata kuwapinga wanaowadhulumu. Ukombozi unaweza kuwa pia ni kukata minyororo ya kiakili inayomfunga mhusika kwa kumzindua au kuzinduka kimawazo mwenyewe.

- Wafanyakazi wanajaribu kujikomboa kwa kuwachagua na kuwatuma viongozi wao kwa Baraza ili kuwasilisha malalamishi yao.

- Wafanyakazi wanagoma Baraza linapokosa kushughulikia shida zao kama njia ya kujikomboa.

- Tatu, Beki na Medi wanamkabili Meya kwa ujasiri na kumweleza malalamiko ya wafanyakazi wenzao.

- Ukombozi wahitaji ujasiri na ukakamavu kwa mfano kufutwa kazi, kupigwa na kuuawa.

- Siki na Diwani III wanatetea maslahi ya wagojwa, maskini na wana Cheneo kwa jumla.

(xxii) **Nafasi ya Mwanamke**

Maudhui ya nafasi ya mwanamke yanahusu masuala ya kijinsia hasa vile ambavyo mhusika wa kike amesawiriwa katika kazi ya kifasihi. Wanawake huwa wanakweza au kutwezwa katika kazi za kifasihi.

Mwandishi wa tamthilia ya *Mstahiki Meya* amewatumia wahusika wachache katika mchezo huu. Hata hivyo, nafasi alizowapa hawa wachache katika mchezo hii. Hata hivyo, nafasi alizowapa hawa wachache zinadhihirisha kwamba, mwanamke hajaachwa nyuma katika shughuli za mapambano katika jamii. Yeye (mwanamke) amejifungata masombo kuhakikisha kwamba haki na usawa vinadumishwa katika jamii kwa minajili ya manufaa ya vizazi vijavyo.

Mmojawapo wa wahusika wa kike ambaye nafasi yake inajitokeza vizuri zaidi ni Waridi. Waridi na Nesi katika hospitali ya Baraza la Cheneo. Wanafanya kazi na wenzake katika hospitali hiyo pamoja na Daktari Siki.

Waridi ni mhusika ambaye anaweza kudaiwa kwamba hajapevuka kamwe kuhusu matatizo yanayokumba nchi yake. Kwake, ukosefu wa dawa pale hospitalini ni jambo linalosababishwa na hali ya nchi yake kuwa changa na maskini (uk.3). Haya si madai wala imani ya kweli kwa kuwa Baraza la Cheneo lina utajiri mkubwa ila tu limeachwa kuongozwa na viongozi walafi.

Ingawa ni mwanamke, ni kinaya kwamba mhusika huyu anamlazimisha mama mwenye mtoto mgojwa kupiga foleni bila kujali kuwa mtoto yuko katika hali mbaya kiafya. Kwa hiyo, tunaweza kudai kwamba hana utu wala huruma (uk.3). Je, adui wa mwanamke ni mwanamke mwenzake katika jamii? Vilevile, anasisitiza kuwa wagojwa wazidi kusubiri dawa na kwamba wanaotaka kulazwa walipie gharama hiyo (uk.7). Hiki ni kinyume na Siki (mwanamume) ambaye anawahurumia wagojwa hao ambao ni mafukara.

Waridi pia anakata tamaa kutokana na hali mbaya ya mambo pale hospitalini. Dawa walizokuwa wakisubiri hazikuletwa. Wagojwa waliendelea kufariki pale hospitalini kutokana na ukosefu wa dawa. Mambo haya yanamfanya kutamauka na kujiuzulu (uk.35). Kwa hivyo, ni mhusika asiyekuwa mvumilivu wala hana stahamala.

Hata hivyo, tukigeuza upande wa pili wa sarafu, kuna mwanamke mwenzake ambaye anapambana bega kwa bega na wanaume katika kukabiliana na dhuluma zinazoikumba jamii. Huyi ni Tatu ambaye sawa na Medi na Beka ni viongozi na wafanyakazi. Wao ndio waliotumwa na wafanyakazi kwenda kuwakilisha mbele ya Meya na kuwasilisha malalamiko yao. Kwa hiyo, katika kiwango hiki, mwandishi amemsawiri mwanamke kama mshirika mwenza wa mwenzake mwanaume katika jitihada za kupigania ukombozi. Tatu ni mtetezi wa haki za wafanyakazi wenzao. Yeye na wenzake wanapofika mbele ya Mstahiki Meya, wanawasilisha matatizo ya

wenzao jinsi walivyotumwa (uk.66-72). Katika kutekeleza hili, wanaonyesha ujasiri na hawachelei kumkosoa Meya. Hawatereki kamwe katika kuutafuta ukweli na wanamwambia Meya ukweli wa mambo yalivyo katika himaya anayoiongoza. Kwa mfano, wanamwambia bayana ukweli kuhusu tofauti za maisha kati ya viongozi (matajiri) ambao ni watawala na maskini (watawaliwa) (uk.69).

Mwanafunzi asome tamthilia na kutambua mifano mingine zaidi kitabuni.

SURA YA NNE

MBINU ZA KISANAA NA MATUMIZI YA LUGHA

Dhana ya mbinu za sanaa inajumusiha mbinu za lugha na zile za uandishi. Fasihi, ingawa hutumia lugha kama malighafi yake, humlazimu mtunzi kuifinyanga kisanaa ili kutofautisha lugha yenyewe na ya taaluma nyingine kama vile historia au hisabati. Mwandishi hufanikiwa kuitia madoido lugha yake kwa kutumia mitindo na tamadhali mbalimbali za lugha.

Mbinu za Uandishi

Mbinu za uandishi ni sawa na mtindo wa mwandishi. Hizi zinahusu upekee wa mwandishi kwa namna anavyoichora kazi yake. Katika tamthilia ya Mstahiki Meya, mwandishi ametumia mbinu zifuatazo;

a) Kinaya

Kinaya ni hali ambayo mhusika anasema au kutenda kinyume na matarajio.

- Anwani 'Mstahiki Meya' ni kinaya kwa sababu Meya amejitokeza kama mhusika ambaye hafai kuheshimiwa hivyo basi hastahiki kama anavyopagazwa jina hilo.
- Uk.14: Meya kusisitiza kuwa malengo ya milenia ndiyo muhimu na kuupuuza mpango wa maendeleo ya miaka kumi muhimu ilhali hayasaidii wananchi.
- Uk.18: Diwani III anapotetea umma anaitwa mchochezi.

- Uk. 19: Jukumu la Bwana Usalama lilikuwa kuwalinda wananchi lakini anatuma askari kuwapiga.

- Uk. 22: Madiwani kuomba wasitozwe kodi na walinda usalama kuongezwa mishahara ilhali Baraza lina nakisi kubwa.

- Uk. 30: Meya kusema kuwa ulimwengu wahitaji watu kama Bili ilhali Bili alizua mipango ya kifisadi.

- Meya amechaguliwa na wana Cheneo, hana nafasi ya kuwaona wala kutatua matatizo yao. (uk.38).

- Uk. 53: Madiwani kujiongeza mishahara, kujiondolea ushuru huku wafanyakazi wanaozalisha pato kwa Baraza wakinyimwa nyongeza, kulipwa mishahara duni na kulipa ushuru huo.

- Uk. 63: Kumtenga Diwani III mwenye ushauri mwema kwa madai kuwa ana wivu na hajui kutunza siri.

- Uk. 63: Diwani I na II kutoa ahadi za kuficha siri ya kuuzwa kwa fimbo ya Meya kama njia ya kulitunza Baraza. Vitendo hivi ni vya kulipunja Baraza wala si kulitunza.

- Uk. 70: Wafanyakazi wa Baraza kukosa kupewa matibabu katika zahanati ya Baraza.

- Uk. 41: Mhubiri kusema uongozi wa Meya utadumu na umebarikiwa ilhali ni uongozi mbaya.

- Uk. 44: Meya kumpa mhubiri ahadi ya sadaka ya shilingi laki moja kila mwezi ilhali baraza lina nakisi na matatizo tele.

- Madiwani kutaka mshahara wa kuwawezesha kuvaa nadhifu huku Baraza limejaa uchafu na ukosefu wa huduma muhimu.

- Uk. 77: Meya wa Baraza hana habari kuwa Baraza halina maji!
- Meya kumpenda Bili na kufuata ushauri wake ilhali Bili anampotosha.
- Meya kuchukulia kifo cha mtoto mmoja kuwa si kitu kwani Cheneo ina watu wengi.
- Meya anakula staftahi ya kifahari huku wafanyakazi wake wakila makombo na chakula cha mbwa.
- Meya kupanga kuwapokea wageni kwa takrima kuu hadi kuagiza vyakula kutoka nchi za nje wakati raia wanakufa njaa na kula chakula kisichofaa binadamu.
- Nyumba ya Meya kunadhifisha huku mji mzima umejaa uvundo.

b) <u>Monolojia/Uzungumzi Nafsia</u>

Monolojia au uzungumzi nafsia ni pale mhusika anajisemea mwenyewe katika tukio fulani ndani ya kazi ya kifasihi.

- Meya anjisemea kwake nyumbani kuhusu viyai pia wakati anapochomwa na chai (uk.8).
- Uk. 25: Meya akiwa ofisini akipanga mikakati ya mapokezi ya Mameya anazungumza pekee kuhusu mapokezi ya kifahari atakayowapa. Aidha kumfurusha mwanakandarasi fulani.
- Uk. 10: Gedi anapomtaarifu kuhusu kuja kwa Siki kasha kuondoka, nakereka na habari za kuja kwa Siki kimonolojia.
- Uk.64-65: Kuna uzungumzi nafsia Dida anapoonyesha namna askari wanavyotumiwa na viongozi kunyamazisha wananchi. Aidha namna waandamanaji walivyouawa.

- Uk. 34: Siki anajisemea kuhusu ushauri aliompa Meya kuwa wananchi wenye njaa ni hatari naye akapuuza.

- Uk. 56: Meya anayarudia peke yake maneno aliyoambiwa na Diwani III kuhusu haja ya kuwasikiliza raia.

c) <u>Vicheko na Ucheshi</u>

- Uk. 64-65: Dida anacheka kicheko kirefu anapojizungumzia kuhusu kazi ya askari na namna waliogoma walivyofurushwa. Ni kicheko cha tashtiti kwa sababu kinaangazia uongozi usiojali malaamishi ya wananchi kiasi cha kuwatoa uhai.

- Uk. 30: Meya anacheka kuonyesha furaha ya mpango mzuri wa Bili kuhusu kugawana hela na mwanakandarasi ili kujitajirisha.

- Kuna ucheshi katika hali ya Meya kudai kuwa ametaka kujiunga na uhubiri mara mbili hivi na anavyosema ameen kwa mhemko.

- Meya na mhubiri wanavyolala chini waliposhtuliwa na askari ni ucheshi. Pia inachekesha kuwa hata Meya anaweza kuingiwa na uoga kiasi kile ilhali alidai hatishwi na yeyote.

- Dida anachekesha msomaji kwa uigizaji na kauli zake kuhusu kazi ya uaskari na jinsi wafanyakazi walivyotorokea maisha yao walipofukuzwa kwa vitoa machozi na bunduki. Kichekesho hiki kinaonyesha namna askari hutumiwa kutekeleza majukumu kwa faida ya kiongozi pasi na kujali wananchi wala kuwa wao wenyewe ni wananchi.

- Uk. 57: Meya anacheka milio ya risasi na sauti za wafanyikazi zinaposikika. Kicheko cha ushindi kuwa askari wamewatawanya wanaogoma.

- Dida anatumia kicheko kirefu anaposawira hali ya Cheneo kwa jumla lakini anacheka kicheko kifupi wakati anadhihirisha kutamauka kwa kuwa hana analoweza kufanya ili kubadili hali.

d) <u>Taswira</u>

Taswira ni istilahi inayotumiwa kurejelea maelezo ambayo yanaunda picha fulani katika akili za msomaji. Kwa hiyo, taswira ni picha ya mawazoni anayoipata au 'kuiona' msomaji anaposoma kazi yoyote ile ya kifasihi – na mumo kwa mumo katika picha hiyo, kunakuwa na ujumbe fulani uliofichika. Taswira huundwa kwa matumizi ya tamathali mbalimbali za usemi, kwa mfano tashbihi na sitiari.

- Mwandishi anapoeleza mandhari ya zahanati anatupa taswira ya daktari akiwa na wasiwasi, foleni ndefu na milio ya watoto.

- Taswira ya kimsha kinywa anachopata Meya katika sebule yenye makochi na zulia la kupendeza inajenga taswira ya utajiri (uk. 8).

- Taswira ya huduma za Gedi kwa Meya kuashiria ubwana na utumwa.

- Taswira ya kitoto kilicholetwa katika zahanati ambacho tumbo lilikuwa kubwa inaashiria utapiamlo.

- Taswira ya Meya na mhubiri wanapokuwa ofisini wakiomba kasha wanashtuliwa na askari na kulala chini kwa woga.

- Uk. 57: Meya akiwa ofisini anaweka faili pembeni anaposikia sauti za wafanyakazi, anawatazama na kurudi kuketi kusoma gazeti bila kujali.

- Uk. 3: Taswira ya mama na mtoto mgojwa na anavyoshughulikiwa na Siki.

- Kuna taswira katika maigizo ya Dida kuhusu kazi ya askari.

- Kuna taswira ya wafanya kazi wanaogoma na namna wanavyofurushwa kwa vitoa machozi na virungu.

e) <u>Majazi</u>

Hii ni mbinu ya mwandishi kuwapa wahusika majina ambayo yanaakisi hulka, tabia na mienendo yao. Jina la mhusika linakuwa kielekezi cha tabia yake. Majazi huhusisha pia majina ya mahali, mandhari. Mbinu hii humsaidia sana msomaji kwa kuwa humwezesha kuifahamu tabia na wasifu wa muhusika kwa urahisi mno. Halikadhalika, kwa kutumia majazi, mwandishi huweza kuchimuza (foreground) mtazamo wake kuwahusu wahusika katika kazi yake. Mwandishi wa fasihi ya Kiswahili aliyetumia mbinu ya majazi kwa ufanisi mkuu ni *Shabaan bin Robert* katika tungo zake kama vile *Adili na Nduguze*, *Utubora Mkulima*, *Kusadikika* na *Kufikirika*. Mtunzi wa tamthilia ya *Mstahiki Meya* pia ametumia mbinu hii kama ifuatavyo:

- Cheneo – lina maana ya kitu kilichoenea au kutapakaa. Katika Baraza la Cheneo hali mbaya imeenea k.m uozo wa maadili. Ubadhirifu, uongo, ufisadi, ukatili na mengineyo ni mfano wa uozo huo. Aidha upo uozo wa mazingira kwa kuwepo taka nyingi zenye kuvunda.

- Bili – ni utohozi wa neno la kiingereza '*bili*' ambayo ni orodho ya vitu vilivyouzwa na kiasi cha fedha zinazodaiwa. Bili ndiye anazua mipango kuhusu kuuza fimbo ya Meya na kupata pesa. Aidha anashauri Meya kujinufaisha fedha kutoka kwa mwanakandarasi ili naye anufaike. Bili pia aliwekwa kwa orodha ya malipo ya Baraza hivyo kuzidisha matumizi ya fedha za Baraza.

- Siki – maji yatumiwayo kuongezea ladha katika vyakula na dawa. Siki ni mhusika anayetia matumaini kwa wagojwa na kutetea wana Cheneo wanaodharauliwa. Anatia ladha katika maisha ambayo vinginevyo yangekuwa yakutamausha. Siki pia ina maana ya uchachu au ukali. Ukali huu unakuwa kero kwa Meya kwa namna anavyomkabili na kupinga maovu anayotenda. Siki anachachuliwa na mazingira ya kazi.

- Kheri lina maana ya bora, utulivu au usalama. Kheri ni kama araka kwa wana Cheneo kwa kuwatetea dhidi ya viongozi dhalimu.

- Dadavuo Kaole – latokana na kitenzi dadavua chenye maana ya kutoa katika tatizo. Kaole linamaanisha kaone. Jina la mtoto liliafiki hali yake iliyohitaji kutazamwa na kutatuliwa na daktari.

- Jina la kijifahari la mkahawa waliozungumzia Meya na Bili lina maana ya kutukuka au ukuu. Hii inarejelea hali ya hawa wawili kutaka kujihusisha na makuu.

- Tatu ni majazi kwa kuwa ni kiongozi wa jopo la wawakilishi watatu la wafanyikazi.

- Bwana Uchumi na Kazi – Diwani anayesimamia shughuli za kazi na pesa.

- Bwana Usalama – Diwani anayesimamia maswala ya usalama.

- Shuara – ni jina la mji ambao ndege zilielekezwa huko badala ya Cheneo. Linatokana na neno shwari lenye maana ya utulivu au usalama basi ukawa salama kwa wageni kuliko ule wa Cheneo uliojaa shaka.

- Sosi – jina la Meya. Sosi ni neno lenye maana ya kula. Tunamwona Meya kwa mara ya kwanza tamthiliani akila sebuleni. Aidha kuna kula kwa kunyakua viwanja na kuungana na Bili na madiwani katika kufisidi Baraza. Sosi pia ni utohozi wa neno '*saucy*' la kiingerza lenye maana ya mchuzi au rojo. Meya anapenda mambo ya kifahari k.m kuitwa kwa jina Mstahiki Meya, kusomesha watoto ng'ambo na mengineo. Sosi pia lina maana ya ujeuri au utundu. Meya ni mjeuri kwa kumfukuza Siki kwake na kukataa pole za Dida. Anadhihirisha utundu kwa kukosa kujali hali ya Cheneo na watu wake.

f) <u>Maswali ya Balagha</u>

Balagha ni mbinu ambapo mwandishi anauliza maswali yasiyohitaji majibu. Maswali ya balagha hivyo basi hayahitaji jibu. Maswali ya aina hii yanadhihirika katika tamthilia ya Mstahiki Meya.

- Uk. 8: Meya anauliza, '*hivi huyu ana nini?*' anapokasirishwa na hali ya chai kumwagika.

- Uk. 10: Meya asema '*ni mpaka uniite Sosi?*' swali analomuuliza Siki ambalo linaonyesha kutofurahishwa na jina hilo.

- Uk. 42: Askari I anashangaa kwa kuuliza, '*Meya?*' Askari II pia anauliza '*wapi?*' maswali waliyouliza wakiwa ofisini mwa Meya baada ya kwenda kule wakidhani Meya amevamiwa. Yanaonyesha kushangaa kwao kuwa waliokuwa wakipiga kelele ni Meya na mhubiri.

- Uk. 55: Meya anamuuliza Diwani wa III, '*wayatakiyani ya mtondogoo?*' kuonyesha hali ya kutojali mambo yalivyo.

- Uk. 61: Bili asema, '*si hiyo dhahabu tupu?*' swali la kushawishi Meya na madiwani kuuza fimbo ya Meya.

- Uk. 70: Tatu akiwa na Meya anauliza '*hospitali hiyo imejengewa kina nani kama si sisi waajiriwa wake?*' swali la kuonyesha hali ya kukerwa na hali ya kukosa huduma za matibabu.

- Uk. 67: Maswali ya Beka na Medi kuhusu kuja kwa wageni. '*Wageni wa siku moja? Wanafanya mtuone sisi kuwa si kitu?*.

g) <u>Kuchanganya Ndimi</u>

Hii ni mbinu ya uandishi ambapo wahusika huzungumza kwa kutumia lugha zaidi ya moja ili kuonyesha hali yao na hisia zao katika mazungumzo. Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* kuna mifano ifuatayo:

- Uk. 5: Waridi anamwuliza Siki '*what do you think this is*? *Food poisoning*?' Anapozungumza kuhusu hali ya mtoto aliyekuwa na utapia mlo. Siki anamjibu, '*oh yes*!'

- Uk. 8: Meya anapochomwa na chai anasema *nonsense*! Analiangalia yai na kusema *bloody hens*!
- Kuitika kwa Gedi kila anapoitwa na Meya ni *yes sir*!
- Uk. 17: *Fridge*
- Uk. 27: *In case, prime plot, entertainment vote*
- Uk. 29: *Gentlemen's agreement, gentlemen's what?*
- Uk. 31: *Talk of the devil*
- Uk. 62: *Full - proof, grand idea*
- Uk. 55: *Insurbodination*
- Uk. 48, 49: *Mayor's Act, Riot Act, Collective Responsibility*

h) <u>Mtindo wa Kishairi</u>

Baadhi ya watunzi wa tamthilia ya Kiswahili hujitahidi sana kutunga michezo yao kwa kuzingatia vigezo sita vya utunzi wa tamthilia alivyoviweka. Aristotle katika kazi yake ya '*The Poetics*', mojawapo wa vigezo hivyo ni wahusika kusema kishairi. Alamin Mazrui, katika *Kilio cha Haki* amefanikiwa sana katika mtindo huu pale ambapo mhusika wake mkuu – Lanina wa Muyaka anasema kishairi. Mtunzi wa tamthilia ya *Mstahiki Meya* pia amewafanya wahusika wake waseme au wazungumze kishairi. Tazama mifano ifuatayo:

- Uk. 34: Maneno ya Siki ambayo yametumiwa kuonyesha ushauri wa Siki kwa Meya.
- Uk. 64-65: Mawazo ya Dida yanawasilishwa kishairi.
- Uk. 57: na uk. 30: Malalamiko ya wafanyikazi na hotuba ya kiongozi wa wafanyikazi zimewasilishwa kishairi.

i) Taharuki

Taharuki ni mbinu inayotumiwa na watunzi wa kazi za kubuni ili kuteka hisia na hamu ya wasomaji. Katika kufanikiwa kujenga taharuki, mwandishi husuka matukio yenye mshikamano na mtiririko ambao humvutia msomaji asiiweke chini kazi hiyo pindi aanzapo kuisoma hadi kikomo chake. Kazi yenye taharuki kubwa haiwezi kumchosha msomaji. Watunzi wa riwaya za upepelezi kama vile Mohamed Said Abdulla na Faraj H. Katalambulla wametumia taharuki ya hali ya juu sana. Mohammed Said Abdulla ameandika riwaya kama vile *Mzimu wa Watu wa Kale, Kosa la Bwana Msa* na *Kisima cha Giningi* huku Faraj H. Katalambulla akitunga *Simu ya Kifo*. Taharuki imejitokeza katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* kwa njia zifuatazo:

- Uk. 25: Meya anasoma faili na kuzungumzia mtu fulani atakayemfurusha hata akishtaki.
- Baada ya kupanga njama ya kuuza fimbo ya Meya, Bili anatoweka hata Meya anapouliza aliko, hakuna aliyejua.
- Mwishoni mwa tamthilia Meya na madiwani wanashikwa naye Meya anazirai ila haibainiki lililofuata.

Simu

- Imetajwa kuwa habari za ndege kuelekezwa mji wa Shuara zinapokelewa na Gedi kupitia simu (uk.76).
- Simu aliyoipokea Siki kutoka kwa Tatu kabla ya kuja kumwona ofisini. Kupitia haya tunaelewa utu na uwajibikaji wa Siki kiasi cha wawakilishi wa wafanyikazi kumtaka ushauri.
- Uk.74-75: Meya anampigia Bili simu lakini ni 'mteja'. Hali hii inaonyesha unafiki wa Bili wa kumshauri vibaya Meya kisha kutoweka.

j) Sauti

- Uk.30: Kuna sauti za wafanyikazi wa Baraza waliogoma. Sauti zinawasilisha mahitaji yao ya kudai maslahi, malipo na huduma za afya bora. Sauti zinalalamikia kudhalilishwa na kupuuzwa.

- Uk.57: Sauti za wafanyikazi zinazodai haki.

- Uk. 57: Sauti ya kiongozi wa wafanyikazi anapowahutubia.

k) <u>Uigizaji</u>

- Uk. 64: Dida anaigiza askari na bunduki yake anarejelea hali iliyotokea ya askari kuwapiga na kuwafukuza wafanyikazi waliokuwa wakigoma.

l) <u>Mbinu Rejeshi</u>

Mbinu rejeshi ni mbinu ya kisanaa ambayo kupitia kwayo mwandishi hurudia mambo yaliyokwisha kusimuliwa hapo mbeleni au awali kupitia mpangilio ya kazi yake au uzungumzi hapo mbeleni au awali kupitia mpangilio ya kazi au uzungumzi nafsia wa wahusika wake. Katika mbinu hii, usimulizi wa matukio huenda mbele na nyuma. Baadhi ya mifano ya mbinu hii katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* ni pamoja na ifuatayo:

- Uk.28: Meya na Bili wanarejelea wakati walijistarehesha katika mkahawa wa Kajifahari.

- Uk. 27: Katika mazungumzo ya Meya na Bili wanataja walivyojigawia ardhi.

- Uk.35: Waridi anarejelea kifo cha binamuye kama sababu mojawapo ya kujiuzulu.

- Uk. 12-13: Meya anataja kuwa amechaguliwa mara tatu mtawalia. Uk.69: Beka anaelezea jinsi mtoto wa Kerekecha alivyokufa kwa ukosefu wa dawa.

- Uk.65: Dida anarejelea mauaji wa wana Cheneo yaliyoendelezwa na askari.

m) <u>Ulinganuzi</u>

Ili kufanikiwa katika kuonyesha tofauti za kitabaka, mwandishi ametumia mbinu ya kulinganisha na kulinganua makundi haya mawili katika jamii ya *Mstahiki Meya*. Kwa mfano:

- Uk. 69: Beka analinganua hali ya wafanyikazi na viongozi k.m. Viongozi wana bima za hospitali ilhali wafanyikazi hawana.

- Wanajiongeza mshahara huku wafanyakazi wakinyimwa.

- Viongozi watumia magari huku wafanyakazi wakitembea.

- Viongozi wanakula vyakula vya thamani nao wafanyakazi wakila vile duni na hata wana wao kufa kwa njaa.

- Uk. 64: Dida analinganua hali na kazi yake na ile ya askari. Anasema kufagia kufagia hakuna heshima na bwana anakutusi ila askari bunduki yake ni mfalme.

n) <u>Lahaja</u>

- Uk. 50: Ndiyo yale ya '*ya ngome in 'tuumiza naswi tu mumo ngomeni*'. Katika Kiswahili sanifu maneno haya ni 'ya ngome inatuumiza nasi tu humo ngomeni'. Katika kauli hii, mwandishi anarejelea dondoo la ushairi wa Muyaka Bin Haji ambaye alikuwa mmoja wa watunzi wa Kiswahili kabla ya karne ya 20 kwa lahaja ya Kimvita.

- Uk. 50: '*Ya mwananti kuivunda nti*' kwa Kiswahili sanifu ni 'ya mwananchi kuivunja nchi'.

o) <u>Takriri</u>

Takriri ni mbinu ya kifasihi ya kurudiarudia jambo ili kusisitiza au kulitilia mkazo.

- Uk. 57: Kuna takriri katika maneno ya wafanyikazi k.m. 'haki yetu, jasho letu'.

- Uk. 32: Kuna takriri katika maneno ya Gedi anaposema, 'wanadai mishahara zaidi; wanadai dawa hospitali; wanadai kukuona; wanadai takriban kila kitu'.
- Uk.64: Maneno ya Dida '*let, rat! Let, rat!*'
- Uk. 68: Maneno ya Beka 'watoto wetu wanahitaji kula, wanahitaji kusomeshwa, wanahitaji maisha'.

p) <u>Jazanda</u>

Jazanda ni mbinu ambayo inaonyesha fumbo lililotumiwa na mwandishi kurejelea hali fulani kwa njia fiche. Jazanda ni tofauti na istiari kwa kuwa istiari inalinganisha moja kwa moja kitu au hali na nyingine lakini jazanda huweka fumbo hilo kwenye muktadha wa kimasimulizi au kurejelea kwa kirefu. Kuna mifano kadha ya jazanda katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*.

Uk. 8 Meya anayepata stafutahi ya vyakula vingi, mayai na chai anapaliwa na yai. Hili inatokea baada yake kubugia yai kwa chai. Anadai mayai ni madogo mno na anaamrisha anayeleta mayai aachishwe mara moja maana yeye akiwa Mstahiki Meya alistahili mayai sio viyai. Yai linalomsakama Meya limetumika kijazanda kwani kawaida yai huwa ni mbegu na hutosha vifaranga. Mayai yasipotunzwa basi vifaranga havianguliwi. Tukirejelea hali ya Cheneo, rasilmali ambazo ndizo nguzo za ustawi wa kiuchumi zinaibwa na kutumiwa vibaya na viongozi.

Meya anapodai mayai makubwa inaonyesha tamaa yake kuu kuifilisi Cheneo. Kule kukatizwa kwa pato la muuza mayai kunadhihirisha hali ya Meya kutojali wafanyakazi na hali zao ilhali wao ndio wenye kuzalisha mali. Kupaliwa na yai kunatabiri hali mbaya ya Meya baada ya uongozi wake mbaya Cheneo hasa pale anapokamatwa na askari.

Isitoshe Dida kumtetea muuzaji mayai, anasema kuwa hali imebadilika na kuku wanataga mayai madogo. Hili linaweza kumaanisha kuwa rasilimali za Cheneo zimepungua kwani wafanyakazi hawajaridhika hivyo hawazalishi mali ipasavyo na ile

kidogo wanayozalisha ina fujwa na viongozi. Jazanda ya utatu pia imejitokeza pakubwa katika tamthilia hii. Kuna vitu vingi ambavyo vinaonekana kuwa ni vitatu. Kwa mfano chai moto ambayo Meya aliyotaka kuteremshia yai pia yaweza kuashiria nyenzo anazotumia Meya kuendeleza uongozi wake mbaya. Meya kwa mfano anatumia kanuni na sheria dhalimu kama *Mayor's Act, Riot Act, Collective Responsibility* na *Entertainment Vote* ili kujifaidi kimapato. Vile vile anatumia asasi ya dini vibaya anapomthamini na kumfadhili kimakosa mhubiri mnafiki jambo linalolifilizi baraza.

Washauri wabaya na vikaragosi wa Meya kama Diwani I na II na Bili hawamsaidii Meya katika utatuzi wa mambo hali inapokuwa mbovu Cheneo. Mhusika kama Bili anatoweka kabisa, anakuwa kama chai moto iliyotakiwa kuteremsha yai lakini inamchoma hivyo anaitema. Ushauri potovu wa hawa washauri ni kama chai moto inayochoma kwani Meya baada ya kuzingatia ushauri wao '*anachomeka*' kwani mwishowe anakamatwa.

Meya anapokasirishwa na mayai madogo anawatukana kuku kwa kutoa mayai madogo kwa kusema, '*bloody hens*'. Kuku wasiofaa ni jazanda ya wafanyikazi, ambao japo wanazalisha mali, Meya anawadharau. '*Bloody*' pia inaweza kuwa inaashiria maafa yanayowafika wana Cheneo chini ya mamlaka ya Mstahiki Meya. Kwa mfano zahanatini watu wanakufa kwa kukosa huduma za matibabu. Aidha wafanyakazi wanaogoma wanauawa kikatili.

Meya anapolitia yai nzima mdomoni ni jazanda ya ulafi wa viongozi kuzifakamia rasilmali za umma.

Shehena ya dawa inayosemekamna kuwa bahari kuu ni jazanda ya suluhisho kutoka nchi za kimataifa ambalo haliwezi kutatua matatizo ya raia wa Cheneo. Fimbo ya mbali haiui nyoka na pia mjenga nchi ni mwananchi na mvunja nchi ni mwananchi. Si ajabu shehena hiyo ya dawa haifiki hadi tamthilia inapofikia tamati.

Jazanda nyingine inayojitokeza tamthiliani ni ile ya malengo ya milenia na mipango ya maendeleo ya miaka kumi. Dhana ya malengo ya milenia inawakilisha malengo ya

kijumla yanayotokana na nchi fadhili na si bainifu na hivyo hayamsaidii mwananchi wa kawaida. Kwa upande mwingine, malengo ya maendeleo ya miaka kumi yanalenga mahitaji ya mwananchi wa kawaida.

Meya Sosi anakwepa haya yanayomfaidi raia wa kawaida na kukimbilia yale ya kimataifa na kujumla ili awafurahishe wafadhili na aweze kufaidi kwa hela atakazoishilia kuzifuja.

Takrima ya wageni ni jazanda inayoonyesha jinsi uongozi unavyotoa kipaumbele kwa masuala ya anasa na starehe huku wakitelekeza yale muhimu ya wananchi kama mishahara, dawa na huduma za kijamii.

Jazanda nyingine iliyotamalaki tamthiliani ni ile tunayoweza kuiita jazanda ya UTATU. Kuna vitu vingi vinavyoonekana vikiwa vitatu tamthiliani. Kwa mfano wanaharakati wanaotetea haki za wafanyakazi wa Cheneo ni watatu na tena wanaoongozwa na mhusika Tatu. Katika malalamiko ya wafanyakazi ni kuwa malipo yao yako nyuma miezi mitatu. Wale madiwani ni watatu. Meya naye aliuza vipande vitatu vya ardhi. Jazanda hii imetumika na mwandhishi Arege kimakusudi ili kukoleza dhana kuwa ulimwengu wa tatu una matatizo mengi. Matatizo ya ufisadi na uongozi mbaya ndiyo wanayofanya ulimwengu wa tatu kubakia nyuma kimaendeleo. Tatu pia ni idadi ya ukamilifu. Tunaona jinsi viongozi wa wafanyakazi wanavyokamilishana katika jitihada zao wakiongozwa na Tatu.

q) <u>Sadfa</u>

Sadfa imejitokeza katika hiyo hiyo idadi ya tatu au utatu. Tatu imejitokeza mahali kwingi tamthiliani. Mwanafunzi atumie maelezo ya jazanda ya utatu kuelezea sadfa ya utatu. Sadfa hii pia ni mbinu ya mwandishi ya kushadidia jinsi matatizo ya ulimwengu wa tatu wamekithiri.

Mbinu nyingine za uandishi alizotumia mwandishi ni pamoja na utohozi na tanakali za sauti.

Mbinu za Lugha

Mbinu za lugha ni sawa na tamathali za usemi. Mbimu hizi hujitokelea katika kauli za wahusika.

a) Methali

Baadhi ya methali zimedokezwa tu.

- Uk. 2: Ngoja ngoja huumiza matumbo. Siki ana maana ya kuwa kuchelewa kwa shehena ya dawa kunahatarisha maisha ya wagojwa.
- Uk. 12-13: Meya anadokezea methali ya 'akili ni nywele, kila mtu ana zake' anaposema, 'akili hii. Walisema ni mali', kuashiria alivyochaguliwa kwa vipindi vitatu mtawalia kwa kutumia mbinu zake za kijanja.
- Uk. 29: Mtumwa hauawi – methali hii inatumiwa na Bili katika kumshawishi Meya kuhusu mpango wa kifisadi na mwanakandarasi.
- Uk. 32: Ni kawaida ya debe tupu kupiga kelele. Bili anadokezea methali ya 'Debe tupu haliachi kutika' kuwarejelea wafanyakazi waliogoma.
- Uk.33: Mbio za sakafuni tu – Bili anadokezea methali, 'Mbio za sakafuni huishia ukingoni kuonyesha kuwa wafanyikazi hawatafaulu.
- Uk.39: Heri nusu shari kuliko shari kamili. Siki anatumia methali hii kumshauri Tatu dhidi ya mgomo kwani wangefutwa au kuendelea kunyimwa mshahara.
- Uk. 45: Lililoandikwa halifutiki. Siki anapomtembelea Diwani III wote wanaitumia metali hii kumaanisha Siki hakutarajia kumkuta nyumbani Diwani III lakini alimpata.
- Uk. 46: Ngoja ngoja hii haisaidii matumbo. Hii imetokana na methali isemayo, 'ngoja ngoja huumiza matumbo. Siki ametumia methali anapozungumzia shehena ya dawa iliyosemekana kuwa bahari kuu japo kwa muda haifiki.

- Uk. 46: Sikio la kufa halisikii dawa. Diwani III anaitumia kumpigia mfano Meya ambaye hatilii maanani ushauri wao.

- Uk. 57: Msiba wa kujitakia kilio kamwe hauna. Meya anatumia usemi hii kutokana na methali, msiba wa kujitakia hauna kilio. Anasema haya anapoona wafanyakazi waliogoma wakipigwa na kukimbilia usalama wao.

- Uk. 58: Mpiga ngumi ukuta hujutia kitendo chake. Usemi huu unatokana na methali, 'mpiga ngumi ukuta huumiza mkonowe'.

- Uk. 77: Asante ya punda ni mateke. Meya anatumia methali hii anapogundua kwamba mhazili amegoma na alikuwa amempendelea kumpa ajira.

Methali nyinginezo katika tamthilia ni pamoja na:

- Uk. 2: Haraka haraka haina Baraka

- Uk.31: Kelele za chura ni kelele tu, hazimzuii ng'ombe kunywa maji. Bili anasema hivi kurejelea unyonge wa wafanyikazi wanaogoma.

- Uk. 39: Heri nusu shari kuliko shari kamili.

- Uk.54: mhitaji siku zote ni mtumwa. Msemo huu unatumiwa na Meya kwa maana ya kuwa wafanyakazi wanaogoma watalazimika kurudi kazini kwa sababu ni wahitaji.

- Uk. 75: Yaliyopita yamepita tugange yajajo.

b) <u>Istiara</u>

Istiara/sitiari ni tamathali ya usemi inayoeleza sifa za kitu kimoja kwa kutumia sifa ya kitu kingine. Ni mbinu ya kiulinganishi ilivyo tashbihi ila ulinganishaji huo haujitokezi waziwazi. Haitumii viungio kama vile 'mithili', 'kama' na 'kadhalika'. Badala yake huhusisha vitu viwili vilivyo na sifa tofauti kabisa – ambapo sifa za kimoja uhamishiwa

kwa kingine. Kwa mfano: Juma ni fisi. Katika mfano huu, sifa za fisi ambazo ni ulafi zimehamishwa kwa Juma. Mifano kutoka kwa tamthilia ya *Mstahiki Meya* ni:

- Uk. 14: Meya anamuonya Siki dhidi ya kumkera au kumchokoza kwa kusema kuwa hilo ni 'kutia kidole katika mzinga wa nyuki'.
- Uk. 14: Siki anamtahadharisha Meya dhidi ya kuwapuuza matatizo ya raia na kuwanyima haki kwa kusema huko ni 'kutembea nyuma ya punda aliyeudhika'.
- Uk. 15: Siki anatumia istiara, 'unamkanyaga nyoka mkia' kumfahamisha Meya kuwa si vyema kukosa kuwashirikisha wana Cheneo katika maamuzi yanayowahusu.
- Uk. 50: Yale ya 'ngome in' tuumiza naswi tu mumo ngomeni' – kutowakabili viongozi waovu wala kutaka kuutwaa uongozi ilhali uongozi huo unawaumiza.
- Uk. 16: Diwani I asema wao ni macho, masikio na sauti ya Meya. Hili linamaanisha kuwa Diwani I na II na Bili wako pale kujali maslahi ya Meya.
- Uk. 33: Bili analinganisha mgomo wa wafanyakazi na mbio za sakafuni kwa maana kuwa juhudi za wafanyakazi hazingefaulu.
- Uk. 62: Meya anawaambia Diwani I na II na Bili wasimfichulie Diwani III siri ya kuuza fimbo kwani yeye 'ni sumu' kwa vile atauchochea umma.
- Uk. 64: Meya anapolinganisha njama ya kuuza fimbo ya Meya na bomu inayoweza kuwalipukia usoni inamaanisha kuwa huu ulikuwa mpango hatari.
- Uk. 17: Diwani wa III anasema kuwa wanafaa kufanya Cheneo 'kuwaka moto wa mafanikio' msemo wenye maana kuwa Cheneo itafanikiwa mno.

c) <u>Misemo</u>

- Uk.14: Kufikia kumi sharti kuanza na moja. Siki anamwambia Meya haya Meya anaposhikilia kuwa malengo ya milenia yalifaa kuliko mpango wa maendeleo wa miaka kumi.

- Uk.30: Mtu haukati mkono unaomlisha. Msemo huu ulitumiwa na Meya kumhakikishia Bili kuwa hangemsahau mpango wa kandarasi ungefaulu.

- Uk. 31: Wasemao mchana usiku watalala. Bili ndiye anayemwambia Meya anaposikia sauti za wafanyikazi wakigoma.

- Uk.49: Mtu huvuna alichopanda. Msemo huu umetumiwa na Diwani III kwa Siki anapozungumzia Meya kuhusu uchaguzi wa viongozi.

- Uk. 61: Kuuma na kuvuvia – Bili anatumia msemo huu kwa Meya na Diwani I na III kuhusu kuficha uovu wao dhidi ya wafanyikazi wageni wasijue kuwa wanafiki.

- Uk. 71: Beka anaposisitiza wayajue, 'tangu utandu hadi ukoko' anamaanisha wajue ukweli wa mambo, bayana kutoka mwanzo hadi mwisho.

- Uk. 16: Fahamu mbivu na mbichi. Diwani III anapotumia msemo huu ana maana kuwa ajue ukweli wa mambo.

Kuna misemo zaidi katika tamthilia kwenye kurasa zifuatazo:

- Uk. 30: Meya asema 'kuwaua ndege watatu kwa jiwe moja' kutokana na msemo wa kiingereza, killing two birds with one stone'.

- Uk. 39: Siki anamwambia Tatu 'msikate tamaa'.

- Uk. 56: Diwani III anakubali kutekeleza anayotaka Meya 'shingo upande'.

- Uk. 13: Siki anaposema babu zetu hawakupigania uhuru tuje 'kusaliti juhudi na ndoto zao ….'

- Uk. 79: Meya anawaambia askari, Diwani I na II 'yote haya mmeyatia chumvi na wanahabari.

- Uk. 45: Siki anamwambia Diwani III, 'nilikuwa ninabahatisha na kumbe kubahatisha ndiko kupata.

d) <u>Tashbihi/Mshabaha</u>

Tashbiha/Tashbihi/Mshabaha ni maneno yanayofananisha kitu, jambo au kitendo na kingine kwa kutumia vihusishi kama vile 'kama', 'mithili', 'ja', 'mfano wa' na kadhalika. Tazama mifano ifuatayo kutoka tamthilia ya *Mstahiki Meya*:

- Uk. 14: Kupinga malengo ya milenia ni sawa na kumkama samba mwenye watoto. Meya anamwonya Siki anapomkumbusha kuhusu haki za wana Cheneo.

- Uk. 45: Bahati kusimama kama mtende. Siki anasema haya baada ya kumpata Kheri kwake nyumbani alipomtembelea. Anaendelea asemapo kuwa uhusiano wake na Meya ni mfano wa mafuta na maji.

- Uk. 47: Cheo ni kama mtoto na chakula. Mlinganisho huu unabainisha hali ya Meya kusahau kubadilika baada ya kupata cheo na kusahau umuhimu wa waliomchagua.

- Uk. 45: Mimi na Meya ni mfano wa mafuta na maji. Siki ana maana kuwa hapatani na Meya.

- Uk. 48: Meya ana uwezo wa kumkunja aliye chini yake kama ua wakati wa alasiri. Diwani III anarejelea uwezo wa Meya kuwadhulumu raia.

- Uk. 48: Diwani III asema kuwa kushindana na Meya ni kama kushindana na ndovu kwa maana kuwa ni jambo gumu.

- Uk. 69: Mtoto wa Kerekecha alikufa kama nzi. Ni tashbihi aliyotumiwa na Beka ili kuonyesha hali ya raia kukosa kuthaminiwa.

e) <u>Tashihisi/Uhuishaji</u>

Hii ni mbinu ya lugha ya kuweka hisia na uhai katika vitu visivyokuwa na uhai.

- Uk. 30: Bahati haifungui milango yake zaidi ya mara moja.
- Uk. 34: Njaa imeangusha miamba.
- Uk. 64: Bunduki inayotema risasi.
- Uk. 65: Magari yanatapika maji.
- Uk. 45: Bahati kusimama.
- Uk. 47: Cheo kumlevya mtu.
- Uk. 20: Uzalendo hauji kwa watu.

SURA YA TANO

WAHUSIKA

Wahusika ni viumbe, wanyama, mizuka, majini au vitu vilivyohuishwa ambavyo vinapewa nafasi ya watu katika kazi ya kifasihi. Wahusika huwa wanaendeleza maudhui katika tamthilia ya Mstahiki Meya.

Meya Sosi - Ni Meya wa nji wa Cheneo.

- Ndiye mhusika mkuu kwa sababu vitushi vyote ama vimejengwa kumhusu au kutokana naye.
- Ni mhusika bapa sugu kwa sababu sifa zake hazibadiliki hadi mwisho wa tamthilia

<u>Sifa.</u>

1. Mwenye hasira/mwingi wa hasira.

- Anapochomwa na chai anashikwa na hasira na kumwita Gedi kwa hasira kasha kudai kuwa Dida ana njama fulani. (uk. 9).

- Anakataa pole zake Dida na kumfokea anaposakamwa na yai.

- Anampa amri Dida kuwa asimruhusu mwenye kuleta mayai, kuleta mayai madogo na kumkatisha kuleta mayai.

- Anakereka na ushauri wa kuhusu hali ya umaskini wa wana Cheneo.

- Anamfokea Siki na kuamwamuru Gedi kumfurusha nyumbani mwake hata kumwambia asije humo tena. (uk.15).

- Diwani III anapotaja kuwa wananchi watataka kujieleza (uk.21) anakasirika (uk.21).

2. Fisadi

- Anakubaliana na Diwani I kuhusu mpango wa kuandaa tamasha na kuwapa vijana zawadi ili kufumba umma macho (uk.20).

- Meya anakubali kushauriwa kubuni kamati wa madiwani ambazo wanachama wake watalipwa pesa nyingi kama hongo ili wanyamaze na wasipinge udhalimu unaoendelea. Anafanya hivi licha ya kuwa Diwani wa tatu anawaona kuwa kuna nakisi au upungufu wa bajeti – wa shilingi milioni mia moja ishirini (uk.22).

- Pia anawaongeza walinda usalama mshahara ili kutekeleza analotaka liwe licha ya baraza kuwa na nakisi hiyo na wafanyakazi walikuwa tayari wanatishia kugoma na hawashughulikiwi kimshahara (uk.22).

- Meya anaonekana kuwa amenyakua vipande vya ardhi na kuviuza vingine na hata kuwagawia wenzake ili kuinua hali yake ya kiuchumi wakati wa shida na huku wananchi wanaumia kwa kukosa huduma muhimu. (uk.27).

- Pia Meya anapanga kwa ushauri wa Bili kufaidi fedha kutoka kwa mwanakandarasi mmoja. (uk.28-30).

- Meya Sosi amekubali mpango wa Bili kuwa wauze fimbo ya Meya na kuuita 'grand idea'. (uk.61-62).

- Watu wanakufa kwa njaa na maradhi ilhali Baraza linatoa 'sadaka' ya laki moja kwa mhubiri kila mwezi na pesa za petrol; huu ni ufisadi mkubwa. (uk.44).

- Meya mwenyewe anakiri ufisadi wake kwa kusema kuwa alimpa mhazili wake kazi licha ya kuwa hakuwa amestahili kazi hiyo.

3. Mbishi / si msikivu/ si mzingativu

- Meya hakubali kuwa hali ni mbaya katika Cheneo anapoambiwa na Siki jinsi watu wanavyokufa kwa ukosefu wa matibabu zahanatini, kukosa chakula na nchi kubaki nyuma kwa jumla. Tunamuona Meya akiwa mkali na kumkaripia Siki na kusema kuwa ametukanwa (uk.14).

- Diwani III anapoelezea hali mbaya ya uchumi ya Cheneo, anashikilia uamuzi wake wa kuongeza mishahara ya walinda usalama (uk.22).

- Hatilii maanani ushauri wa Diwani III kuwa Baraza halina pesa ila anatoa maamuzi kwa kumpuuza hata kama anafahamu kuwa nakisi ya shilingi 120 milioni (uk.22).

- Diwani III anamshauri dhidi ya swala la kuajiri wafanyakazi wapya anasema ni 'insurbodination' (uk.54-55).

4. Mwenye kiburi

Kiburi ni maringo, majitapo, kujinaki na kutokuwa mnyenyekevu.

- Anapuuza ushauri wa Siki na kudai kuwa watu bado watamchagua hata mara ya nne kama walivyofanya mwanzoni. (uk.12)

- Hajali kuwa watu wana njaa mradi nyoyo zimeridhika. (uk.13)

- Siki anapotaja kitoto kufa anashangaa kuwa kitoto kimoja tu ilhali Cheneo nzima ina watu wengi wanaomuunga mkono. (uk.12).

- Anadharau mfumo wa elimu wa Cheneo kuwa ni mwovu na hauwafai watoto wake. Pia anawadharau madaktari waliosomea Cheneo kuwa hawana ujuzi kama wa ng'ambo. (uk.26-27).

- Meya anataka mwanawe awe raia wa ng'ambo – anadharau uraia wake. (uk.27)

- Sosi anawachukulia wafanyikazi kuwa wahitaji hivyo basi watumwa. (uk.54).

5. Mwenye mapuuza au mtu asiyewajibika

- Baraza limejaa uchafu kiasi cha kunuka ilhali hajali anapoambiwa na Gedi kuwa harufu mbaya inatokana na uchafu huo. (uk.18-19).

- Kuna migomo ya wafanyakazi na malalamishi kuhusu uongozi wa Baraza. (uk.31, 66-72).

- Meya amewapuuza watu wa Cheneo wakifa na tunaona yeye hafikiki kwa kuwa anadai kuwa diary imejaa (uk. 34).

- Anatoa ahadi asizozitimiza k.m. kuhusu uagizwaji wa dawa zahanatini. (uk.38)

- Anapoambiwa kuwa wafanyakazi wamegoma hajali, asema wagome tu na anatishia kuwafuta kazi wote na kuwaajiri wengine. (uk.210)

6. Katili/ hana utu / mwenye unyama

- Tunamwona akimfukuza Siki, ambaye ni binamu yake kutoka nyumbani kwake. (uk.15)

- Anavyowaamrisha wahudumu wake kwa mfano Gedi na Dida. (uk.8-10, 15, 17-19, 31-33, 42-43).

- Anatumia askari wake kuwapiga wafanyakazi wanaogoma. (uk.57).

- Meya pia hajali kifo cha kitoto alichotajiwa na Siki kuwa kimeaga. (uk.12).

7. Mbadhirifu

- Anapokubali kuongeza mishahara ilhali baraza lina nakisi ya shilingi mia moja na ishrini milioni (uk.22)

- Anapanga mapokezi ya kifahari kwa wageni ilhali baraza halina hela.

- Anauza vipande vya ardhi vitatu alivyonyakuwa na pia tunamuona akitumia pesa za umma kumpeleka mkewe kujifungulia ng'ambo na watoto wake kusomea ng'ambo.

- Anazitumia hela za Baraza kujistarehesha yeye, Bili na familia yake. (uk.27)

<u>Umuhimu wake</u>

- Kielezo cha namna viongozi wanavyojali maslahi yao na kutozingatia hali ya nchi na wananchi wake.

- Kutokana naye, tunaangaziwa kuwa uongozi mbaya huwa na hatima mbaya.

- Anatumiwa kuonyesha athari za uongozi mbaya.

- Ni wakilisho la jinsi ulafi na ubinafsi wa viongozi vinavyoweza kudhuru nchi na wananchi.

- Ni kioo cha uozo ulivyokithiri katika taasisi za serikali katika nchi za Afrika.

<u>Siki</u>

- Ni daktari ambaye pia ni binamuye (Meya)

- Ni daktari katika zahanati ya Baraza la mji wa Cheneo.

<u>Sifa zake</u>

a) <u>Mwingi wa utu</u>

- Anamhurumia mama mwenye mtoto mgojwa pale hospitalini na kumhudumia wakati Waridi alikuwa amemkemea.

- Hali ya ukosefu wa dawa katika zahanati inamtia wasiwasi na kumfikirisha mno. (uk.1-2)

- Waridi anapolalamika kuwa wagojwa hawana karatasi, Siki anawatetea kuwa hawana pesa.

- Ana hiari kuwalaza wagojwa hospitali alimradi kuwapa tumaini.

- Anamzuru Meya ili kumfahamisha namna hali ilivyodorora Cheneo kwa kuwa anawaonea huruma raia wanavyoteseka kwa kukosa huduma muhimu. (uk.10-15)

- Yukoadhi kuteseka na wagojwa wakati Waridi anapoamua kujiuzulu na kuondoka zahanatini. (uk.36)

b) Anawajibika

- Yuko tayari kuwashughulikia wagojwa ambao dawa zao zinapatikana zahanatini (uk.2).

- Anashauri Waridi kuandaa mchanganyiko wa kusaidia mtoto mwenye utapiamlo. (uk.6).

- Anachukua jukumu la kumzuru Meya ili kumbainisha hali duni inayowakumba wana Cheneo na kumshauri dhidi ya uongozi wake mbaya. (uk.10-15).

c) Mdadisi /mwenye makini

- Anamhoji Waridi kuhusu shehena za dawa zinazosemekana kuwa zimeagizwa na ziko katika bahari kuu (uk.2).

- Tunamuona akijadili kwa kina na Diwani III kuhusu masuala ya kijumla yanayokabili Cheneo na kuonyesha uelewa mkubwa wa mambo. (uk.45-51).

- Anamhoji mama mwenye mtoto mgojwa kwa makini kuhusu ugojwa wa mwanawe.

Asiyetamauka / hakati tamaa kwa haraka/mvumilivu

- Hali inapokuwa si hali pale zahanatini anajikaza kuokoa maisha ya mtoto kwa namna mbadala ya kumchanganyia sukari na chumvi katika maji ya moto. (uk.3).

- Waridi anapoelekea kuwa hana tumaini kwa wagojwa, Siki anamhimiza kuwa walazwe ili wapate matumaini. (uk.6).

- Anatumainia kuwasili kwa shehena ya dawa licha ya kuwa hafahamu zaidi kuhusu habari zake hiyo.

-Anamshauri Waridi kuwa hali ikibadilika mshahara utabadilika wakati Waridi anatishia kujiuzulu (uk.36).

- Anapanga kuzungumza na Bwana Fedha na Kazi licha ya kuwa Meya hakumsikiza kuhusu matatizo ya Cheneo (uk.45-51).

- Anamtahadharisha Kheri (Diwani III) dhidi ya kukata tamaa na kumkumbusha Meya Sosi wajibu wake kama kiongozi (uk.50).

d) Mshauri mwema

-Anashauri Tatu kuhusu madhara ya mgomo kuwa watu wanaweza kufutwa kazi. (uk.38-39)

- Anamshauri Tatu kutumia nafasi ya kuja kwa wageni kushirikisha Meya kukutana nao. (uk.39-40).

- Ndiye aliyempa Waridi ushauri wa kumpa mtoto mgojwa mchanganyiko wa maji chumvi na sukari. (uk.6)

-Anamshauri Meya dhidi ya kupuuza matakwa ya wana Cheneo. (uk.12)

- Anashauriana na Kheri kwa kirefu kuhusu Meya na namna ya kumshawishi (uk.45- 51).

- Anampa Kheri ushauri wa kuendelea kumshauri na kumkumbusha Meya matatizo ya wana Cheneo. (uk.45-51).

Umuhimu wa mhusika Siki.

- Anatuonyesha haja ya ukakamavu katika kutatua matatizo yanayoikumba nchi.

- Yeye ni kielelezo cha mfanyakazi anayewajibika kazini na kwa jamii.

- Siki ni mfano mwema wa utu usiopingwa au kufifishwa na hali yoyote.

- Ni kielelezo cha maadili na uongofu katika jamii hasa tunapomuona akiishi na kufuata msimamo wake bila kusukumwa na mamlaka na uozo wa binamuye Meya.

Waridi

- Nesi wa hospitali ya Baraza la Cheneo.

Sifa zake

1. Mwenye kutamauka/kuvunjika moyo haraka

- Anakata tamaa kuhusu hali mbaya hospitalini na kujiuzulu au kuacha kazi. (uk.35- 36)

- Hakuwa na tumaini la kuwalaza wagojwa kwenye hospitali isiyo dawa. (uk.6)

- Haoni tumaini la kulipwa mshahara licha ya kushawishiwa na Siki. (uk.36)

2. Anapenda kulalamika

- Analalamika kuhusu kifo cha binamuye (uk.35-36)

- Analalamika kuhusu hali duni zahanatini (uk.36)

- Analalamika kuletewa wagojwa wa utapiamlo kutibiwa zahanatini na dawa hakuna (uk.5-6).

- Analalamika kuhusu mshahara duni na usiolopwa kwa wakati. (uk.36)

3. Mkali

- Anamkemea mama aliyejitoma ofisini na mtoto mgojwa. (uk.3)

<u>Umuhimu wa mhusika Waridi</u>

- Anawakilisha maoni ya Meya ambayo ni ujanja wa Meya kuhusu dawa.

- Anasaidia kuelewa hali duni ya zahanati za umma ambazo husababisha hata vifo kwa mapuuza ya wahudumu kama wauguzi na madaktari.

- Anasawiri masaibu ambayo wahudumu za zahanati hupitia.

- Anawakilisha wafanyakazi wanaotoroka hali duni za kazi na kuenda kutafuta kazi bora kwingineko.

<u>Bili</u>

- Rafikiye Meya Sosi (Mstahiki Meya)

<u>Sifa zake</u>

1. Mfisadi

i) Anazua mpango wa kupata hongo toka kwa mwanakandarasi.

ii) Anashauri kuuzwa kwa fimbo ya Meya.

iii) Aidha anatoa wazo la kutumia propaganda kuwa fimbo imeibwa ili isidadisiwe.

2. Mshauri mbaya

i) Anachangia maoni ya Meya kuwa elimu ya huku ni ya akina yakhe.

ii) Anashauri kuuza fimbo ya Meya kujipatia pesa.

iii) Anashauri kutumia uongo kuzuia udadisi.

iv) Anamhimiza Meya kuwa wanaogoma ni mbio za sakafuni tu.

3. Mnafiki

i) Anampa Meya ushauri mbaya wa kumtia shimoni na hatimaye anamtoroka mambo yanapotumbukia nyongo.

<u>Umuhimu wa Bili</u>

i) Anatumiwa kuonyesha hila na ujanja wa viongozi katika mipango yao.

ii) Kielelezo cha washirika wa viongozi katika kupunja nchi.

iii) Anaendeleza hali ya kashfa za kifisadi zinazopangwa na viongozi.

<u>Diwani III</u>

- Jina lake ni Kheri
- Ndiye kinara wa Uchumi na Kazi katika Baraza la Cheneo.

<u>Sifa zake</u>

1. Mwerevu

-Anamshauri Meya kuwa wabuni mikakati ya kuongeza pato la Baraza badala ya kujiongeza mishahara wenyewe. (uk.54)

- Madiwani wenzake wanakubali kila analolisema Meya ila yeye tu anayetaka na kuuliza maelezo zaidi na kusaili ufafanuzi.

- Anatambua na kufahamisha wenzake kuwa watu wameerevuka na propaganda hazitawahadaa kukubaliana na udhalimu wa Meya.

- Anasisitiza kuwa wafanyakazi na madiwani wote ni watoa huduma kwa umma.

- Anawakumbusha madiwani wenzake na pia Meya kuhusu haja ya kusikiliza vilio vya watu na wafanyakazi.

2. Jasiri

- Anamkabili Meya kwa kutomshirikisha katika kikao kilichoidhinisha ongezeko la mishahara ya madiwani.

-Anamdadisi Meya iwapo ana hakika ya madai kuwa kuna madiwani wachochezi (uk.18).

-Anamwuliza Meya sababu ya kuwaita mkutanoni.

- Anamhoji Meya kufuatana na uongo kuhusu uagizaji wa dawa.

- Anapinga ongezeko la mishahara wakati Baraza lina nakisi.

3. Mtetezi wa haki

- Kusisitiza kuwa wananchi wasipewe ahadi ambazo hazitimiziki.

- Meya anapodai kuwa uchumi umeimarika anapinga kwa sababu wananchi hawajafaidi.

-Anamkumbusha Meya kuwa wametumwa kuwakilisha watu.

4. Mkakamavu

- Hakufa moyo kwa kupuuzwa na Meya, aliendelea kumwambia ukweli.

- Anamwambia Siki kuwa hajakata tamaa kuzungumzia Meya.

Umuhimu wake

- Kuwakilisha viongozi waadilifu na wenye nia ya kuboresha nchi.
- Anatumiwa kumulika ujasiri chanya ambao ni muhimu katika kubadili hali kandamizi na ambazo hazifai katika jamii.

Diwani I na Diwani II

- Diwani I – Kinara wa Maswala ya Usalama.
- Diwani II – Kinara wa Uhusiano Mwema.

Sifa zao

1. Ni vibaraka au vikaragosi

- Wanakubali kila asemalo Meya bila kuuliza maswali k.m. anapodai kuna uchochezi (uk.18)
- Kutumiwa kunyamazisha wananchi kwa kutumia polisi (Diwani I).
- Kushauri kuwa wachochezi wachukuliwe hatua (Diwani II).
- Kuunga Meya mkono kuwa wanaogoma wafutwe kazi (Diwani I).
- Ni ujinga kutaka madiwani waongezwe mshahara ili wamudu mavazi bora.

2. Wanafiki

- Anashauri vijana waandaliwe tamasha na kupewa zawadi ndogondogo (Diwani I)
- Mashindano yaonyeshwa kwenye runinga kama mbinu ya kufumba macho (Diwani II)

3. Wabinafsi

- Wanajali hali zao kwa mfano kuongeza mshahara ili wamudu mavazi bora.
- Wanaafikiana katika kusisitiza kuwa uchumi umeimarika basi waongezwe mshahara.

<u>Umuhimu wa Diwani I na II</u>

- Vibaraka wa viongozi ambao hawajali maendeleo ya nchi ila kuwapigia debe viongozi.
- Wanachangia kuvunja kwa kuwaunga mikono viongozi wabaya.

SURA YA SITA

JINSI YA KUJIBU MASWALI

Kuna aina mbili ya makundi ya maswali ya fasihi yanayotahiniwa na Baraza la Taifa la Mtihani la Kenya (KNEC) katika mtihani wa Kenya Certificate of Secondary Education (KCSE). Makundi haya ni pamoja na

a) Maswali ya muktadha au dondoo

b) Maswali ya insha.

a) <u>Maswali ya Muktadha au Dondoo</u>

Kundi hili la maswali hulenga kutathmini au kupima uwezo wa mwanafunzi kuelewa kwa kina sehemu fulani au kifungu cha matini (text) kutoka kwenye hadithi. Katika muktadha huu, matini ambayo kwayo mwanafunzi atatahiniwa ni tamthilia ya *Mstahiki Meya*. Kwa hivyo, ni muhimu mwananfunzi aonyeshe kuwa anafahamu kwa kina sehemu zilizolengwa na swali; pamoja na kuonyesha ufahamu wa kulinganisha na kulinganua dondoo husika na sehemu nyingine kwenye hadithi.

Mara nyingi, maswali ya dondoo au muktadha humhitaji mtahiniwa atoe ufafanuzi kuhusu maneno yaliyodondolewa. Je, yalisemwa na nani au kina nani? Walikuwa wakiambiwa akina nani? Walikuwa wapi? Ni kitu gani kilichotangulia kauli au usemi huo? Ni kitu gani kilichofuatia tamko hilo?

<u>Mifano ya maswali ya muktadha au dondoo.</u>

1. **"Hata Bwana aliteswa kwa sababu ya neno. Mateso yake yalikuwa makubwa. Hayawezi kulinganishwa na tendo hili dogo".**

a) Fafanua muktadha wa dondoo hili.

b) Eleza ni kwa nini anayeambiwa kauli hii analinganishwa na "Bwana".

c) Msemaji anazungumzia tendo gani analoliita dogo?

d) Toa idhibati kuthibitisha ukweli kwamba msemaji ni mtu mwenye sifa za unafiki katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*.

2. **"Ni …. habari za duru za kuaminika Mstahiki. Tena kuna madai kuwa wageni wanaogopa kuwa huenda ugojwa wa kipindupindu ukazuka. Wanaogopa mkurupuko wa kipindupindu …."**

a) Fafanua muktadha wa maneno haya.

b) Ni nini kilichofuatia kauli hii.

c) Ni kwa nini kuna hofu ya kuzuka kwa maradhi ya kipindupindu?

3. **"Mimi na Meya ni mfano wa mafuta na maji".**

a) Ni nani aliyasema maneno haya? Aliyasema akimwambia nani? Kwa nini? Hawa wana uhusiano gani?

b) Maneno haya yatuonyesha nini kuhusu tabia ya anayeyasema na anayesemeshwa?

c) Ni nani ‘mafuta’ na ni nani ‘maji?’. Kwa nini?

4. **“Sina pingamizi maana hii ni grand idea. Lakini kwanza mniahidi hili mtakwenda nalo kaburini”.**

a) Eleza muktadha wa dondoo hili.

b) Fafanua matumizi yakauli grand idea katika muktadha wa dondoo hili na ueleze ni jambo lipi lilikuwa linarejelewa.

c) Taja na kueleza mbinu anaposema kuwa, “maana hii ni grand idea”.

d) Ni kwa nini msemaji anawasihi wenzake wajitayarishe kwenda kaburini kwa kuihifadhi siri ya jambo hili?

e) Mpango unaorejelewa kwenye dondoo hili unahusu nini?

b). <u>Maswali ya insha.</u>

Kundi hili la maswali humhitaji mwanafunzi au mtahiniwa kutalii kwa marefu na mapana matini nzima ya hadithi. Aidha, maswali ya insha huweza kumpa fursa mtahiniwa kuonyesha ujuzi wake wa kudadisi, kuhoji na kufungamanisha vipengele kadha vya kazi ya kifasihi; mathalan wahusika, maudhui, mbinu za matumizi ya lugha na kadhalika. Haya yote hutekelezwa kwa kuandika mtungo au insha. Suali la insha huwezesha mwanafunzi kuonyesha jinsi anavyoweza kubainisha uzi unaovifungamanisha vipengele mbalimbali vya kazi ya fasihi; kwa kupanga hoja zake kwa aya na kuonyesha muumano ulioko.

<u>Mifano ya Maswali ya Insha</u>

1. ‘Tamthilia ya *Mstahiki Meya* inaakisi hali halisi katika mataifa mengi ya bara la Afrika’. Jadili kauli hii huku ukitoa mifano mwafaka kutetea hoja zako.

2. ‘Tamthilia ya *Mstahiki Meya* inaakisi hali halisi ya mapambano ya kitabaka katika jamii’. Fafanua.

3. Tathmini chanzo cha matatizo yanayolikumba Baraza la Cheneo na upendekeze jinsi yanavyoweza kutatulia.

4. Ufisadi na ubadhirifu wa fedha za umma ni maradhi makubwa katika jamii. Fafanua kauli hii kwa kurejelea tamthilia ya *Mstahiki Meya*.

5. Fafanua maudhui kuu yanayojitokeza katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*.

6. Mtunzi wa *Mstahiki Meya* amefanikiwa sana katika mbinu za kisanaa alizotumia kuisimulia hadithi yake. Jadili rai hii huku ukitoa mifano mwafaka kutoka kwenye tamthilia.

7. Eleza kwa kina sababu zilizochangia migomo katika himaya ya *Mstahiki Meya*.

8. Ukaragosi ni sumu mbaya sana katika uongozi wa mataifa yoyote yawayo duniani. Jadili kauli hii kwa kurejelea tamthilia ya *Mstahiki Meya*.

9. Fafanua migogoro mikuu inayojitokeza katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*.

10. Ukoloni mamboleo bado unatatiza maendeleo ya mataifa ya Afrika. Fafanua rai hii kwa kurejelea tamthilia ya *Mstahiki Meya*.